# Nipashe

Jumatatu Septemba 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581794

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Nipashe Spotika

LUIS SUAREZ ... UKURASA 14

VINICIUS BELLINGHAM MBAPPE

NYOTA 5 WENYE NAFASI KUBWA YA KUTWAA BALLON D'OR 2024

ISIKUPITE

UKURASA 11

**Wananchi** 3,600 kulipwa bilioni 46/- kupisha ushoroba



UKURASA WA 4

**Baraza** la Mawaziri kivuli ACT Zanzibar lazua jambo



UKURASA WA 17

**Tume** yatoa ripoti uchunguzi madai mgodi wa North Mara kunyanyasa wananchi Tarime

UKURASA WA 19

## KADA ALIYETEKWA ...

# CHADEMA, askari polisi wavutana mochwari



• **Mbowe:** Mwili una majeraha, ulimwagiwa tindikali, tutafungua kesi mahakamani... *Ukurasa 2*



Wafanyabiashara wa mazao na makuli mkoani Singida wakiwa wamefunga barabara kuu ya Dodoma-Singida-Mwanza juzi eneo la uwanja wa mpira wa Liti, mjini Singida wakipinga Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wafunga barabara kwa magogo kupinga stakabadhi ghalani

UKURASA 2

UKURASA WA 3

## MAKALLA: WANANCHI WAOGOPENI WANASIASA WENYE UCHONGANISHI

UKURASA WA 3

## WATUHUMIWA MAUAJI MAMA, MWANAWE WANASWA NA POLISI

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya mama Mwamvita ...

# Mtatiro amjibu Askofu Bagonza

UKURASA 10

**MICHEZO** GAMONDI ASHTUKIA KITU LIGI KUU, CAF UK.24 **MAONI,** UK.6

# Wafunga barabara kupinga mfumo stakabadhi ghalani

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAFANYABIASHARA wa mazao na wabeba mizigo mjini Singida wameandamana na kufunga barabara kuu ya Dodoma-Singida-Shinyanga kwa magogo na miti wakipinga mfumo wa stakabadhi ghalani.

Maandamano hayo yalifanywa juzi, wakifunga barabara kwa muda wa saa moja katika eneo la Uwanja wa Liti baada ya kukamatwa magari yao ambayo yalikuwa yamebeba mazao waliyonunua kutoka vijijini; kwamba serikali ilitaka wakayauze kwa mfumo huo.

Hata hivyo, askari wa Jeshi la Polisi mkoani Singida walifika katika eneo hilo na kuwatawanya wafanyabiashara hao na kufungua barabara hiyo.

Wakizungumza na Nipashe, wafanyabiashara hao, akiwamo Abubakari Francis, walisema mfumo wa stakabadhi ghalani ni mzuri, lakini una upungufu kwa sababu wananchi hawajapewa elimu ya namna ya kuuza mazao yao.

Mfanyabiashara Mohamed Nassoro alisema utaratibu wa kuuza mazao kwa kutumia mfumo huo usitishwe kwanza msimu huu, ili serikali itoe elimu kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alifika eneo hilo na kueleza kuwa uuzaji mazao kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani umeleta mapinduzi makubwa katika biashara ya mazao mkoani mwake.

Akitoa mfano, Halima alisema bei ya dengu imepanda hadi kufikia Sh. 2,060 kwa kilo na kwamba utaratibu huo umepunguza changamoto zilizokuwa zinawakumba wakulima kama vile upotevu wa mazao, bei duni na unyonyaji kutoka kwa wafanyabiashara.

Halima alisema: "Kumekuwa na ongezeko la bei ya dengu ambapo awali zilikuwa zinauzwa kati ya Sh. 900 na1,300 kwa kilo. Katika msimu wa 2023/24 na sasa inauzwa kati ya Sh. 1,670 na 2,060 kwa kilo."

Alisema kuwa kutokana na mafakikio hayo, serikali mkoani Singida itaendelea kuhamasisha wakulima kutumia mfumo huo kwa faida ya maendeleo ya kilimo na uchumi wa taifa.

Alisema pamoja na mafanikio katika kutumia mfumo huo, kumekuwa na changamoto kadhaa kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kutokubaliana na mfumo huo kwa madai hawapati faida kubwa ambayo walikuwa wanapata awali.

Halima alisema kuwa kutokana na kuongezeka kwa bei ya dengu, mapato ya halmashauri pia yameongezeka, wamedhibiti utoroshaji mazao hali iliyowezesha serikali kuwa na uhakika wa takwimu, urahisi wa mikopo kwa wakulima na kuongezeka kwa masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi.

Mkoa wa Singida ulizindua rasmi utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu 2024/25 kufuatia maagizo yaliyotolewa na serikali kupitia mwongozo wa biashara ya dengu, mbaazi na ufuta.

Mwongozo huo ulitolewa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa (TMX).


NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI -MWANZA- SHAURI LA JINAI Na.176/2012
ZAINABU GILALA ...........................................1st APPLICANT/OBJECTOR
REHEMA FADHILI MASAWE ............................ 2nd APPLICANT/OBJECTOR
DHIDI YA
REPUBLIC
WAINDI CLEOPHACE (COURT BROKER) } ______________RESPONDENTS
RAJABU MAGOTI

M/MWANZO YA ILEMELA - SHAURI LA MADAI Na. 32/2023

VEDASTUS MNUBI MAKENE ______________________MDAI
DHIDI YA
HASSAN ABDALLAH UKWAJU ____________________MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI-MWANZA, MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA, TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI AMBAZO NI NYUMBA MBILI (3). MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 01 | NYUMBA 01 PLOT No.84 BLOCK'L' SENGEREMA – DISTRICT, PAMOJA NA NYUMBA PLOT No.208 BLOCK 'A' NYAKATO AREA –MWANZA CITY. | SENGEREMA DISTRICT, PAMOJA NA NYAKATO AREA MWANZA CITY. | 09/10/2024 SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 02 | KIWANJA NA.04 BLOCK 'K' CHENYE NYUMBA NA.IGM/KLM/653 KILICHOPO IGOMA NYAMAGANA- MWANZA | IGOMA NYAMAGANA - MWANZA | 16/10/2024 SAA 02:00 ASUBUHI NA KUENDELA |

MASHARTI YA MNADA;
1. KWA MALI INAYOHAMISHIKA, MSHINDI WA MNADA ATALIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA MARA BAADA YA KUTANGAZWA MSHINDI.
2. KWA MALI ISIYOHAMISHIKA, MSHINDI ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
3. MTEJA ANATAKIWA KUKAGUA MALI KABLA YA MNADA KUANZA.
4. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

MAWASILIANO: 0768-588155




RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akiongoza ujumbe wa Tanzania katika mazungumzo na Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi (kulia ) akiwa na ujumbe wake mazungumzo yaliyofanyika Ikulu, Maputo, Msumbiji mwishoni mwa wiki. **PICHA: IKULU**

# CHADEMA, polisi wavutana mochwari

**Na Jenifer Gilla**

KADA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ally Kibao, aliyedaiwa kufungwa pingu kisha kushushwa katika basi Ijumaa iliyopita mkoani Dar es Salaam, amepatikana akiwa amefariki dunia.

Kukiwa na utata kuhusu chanzo cha kifo cha Mjumbe huyo wa Sekretarieti ya CHADEMA Taifa na Msaidizi wa Katibu Mkuu, jana kulitokea mvutano mkali kati ya viongozi wa CHADEMA na Jeshi la Polisi kwenye mlango wa chumba cha kuhifadhi maiti (mochwari) cha Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala ulikohifadhiwa mwili wake.

Kibao anadaiwa kuwa jioni ya Septemba 6 mwaka huu, maeneo ya Kibo Complex Tegeta, Dar es Salaam, akiwa safarini kuelekea nyumbani kwake Sahare, mkoani Tanga na basi la Tashrif, alishushwa katika basi hilo na watu waliokuwa na bunduki.

Juzi Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime alisema wanafuatilia tukio hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala walikokwenda kutambua na kufanyia uchunguzi mwili wa marehemu, Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema wanatarajia kufungua kesi ili ukweli wa jambo hilo ufahamike na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Mbowe alisema uamuzi wa kufungua kesi umekuja baada ya kujiridhisha kuwa Kibao aliuawa.

Alidai kuwa hata mazingira ya kuchukuliwa kwa kada wao huyo yanaonesha kuwa alichukuliwa na vyombo vya dola kwa sababu mashuhuda waliokuwapo, waliwaona watu hao walikuwa wameshika silaha za moto (bunduki) wakiingia katika basi na kumchukua.

"Sisi kama chama tunaendelea kushauriana viongozi pamoja na familia ili katika hatua za baadaye tuone tunaweza kuchukua hatua gani za kisheria kwa sababu mtu huyu ameuawa na hatuwezi kuruhusu hali hii ikaendelea," alisema Mbowe.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa za kifo, walishauriana na ndugu wa marehemu na kukubaliana na mwanasheria wa chama ashiriki katika kufanyia uchunguzi mwili.

Alisema matokeo ya uchunguzi yameonesha kuwa Kibao aliuawa kwa kupigwa na kumwagiwa tindikali usoni.

"Sasa polisi ambao ndiyo watuhumiwa namba moja katika jambo hili na ndiyo wenye wajibu wa kulinda watu wa taifa hili, ni vigumu wao wenyewe kujichunguza, hivyo tunahitaji polisi pamoja na vyombo vingine vya usalama watoe ushirikiano kwa chama na familia, ili haki ipatikane na waliohusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Mbowe alisema kuna mambo mengine ambayo bado yanafanyiwa uchunguzi na wanasubiri taarifa rasmi ya hospitali ambayo inatarajiwa kutolewa leo.

Alitoa angalizo kuwa kama taarifa hiyo itakuwa tofauti na vile wanavyotarajia, wataipinga kwa kuwa mawakili wa chama chao wanajua ukweli kwa kuwa walishiriki katika hatua zote za uchunguzi.

Mbowe alitoa pole kwa familia ya marehemu, ndugu jamaa na marafiki na wanachama wa CHADEMA kwa kupata msiba huo.

Wakati uchunguzi wa mwili wa marehemu ukiendelea katika chumba cha kuhifadhi maiti hospitalini huko, vilio na majonzi vilisikika kutoka kwa wanachama wa chama hicho.

Baadhi ya wanachama walisikika wakitoa lawama kwa Jeshi la Polisi, wakidai linahusika na vitendo vya kikatili dhidi ya wanachama, wanaharakati na Watanzania.

**VURUGU MOCHWARI**

Ilipotimu saa 6: 56 mchana, kulitokea mvutano mkali baina ya polisi waliokuwa ndani ya chumba cha kuhifadhi maiti na viongozi wa CHADEMA, akiwamo aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob.

Mvutano huo ulidumu kwa takribani dakika 20 baada ya madaktari kumzuia Mwanasheria wa CHADEMA kuingia ndani ya chumba hicho, wakidai kuwa tayari kulikuwa na mwanasheria mwingine ndani ya chumba hicho.

CHADEMA ilipinga kauli hiyo na kusisitiza kuwa hawamfahamu wakili aliyekuwa ndani ya mochwari, kwamba wakili wao ni yule aliyesimama nje ya mlango.

Baada ya mvutano huo, uongozi wa hospitali pamoja na polisi walimruhusu wakili huyo kuingia ndani.

Chama cha ACT Wazalendo kimelaani taarifa za kutekwa na kuuawa kada huyo, kikisema kitendo hicho kinahusishwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Kupitia taarifa kwa umma iliyotolewa na chama hicho jana, Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani, Dahlia Hassan alieleza kuwa chama hicho kimepokea kwa masikitiko taarifa hizo; kifo cha kada huyo kinaongeza idadi ya matukio ya utekaji, utesaji na mauaji ya raia nchini ambayo yanahusishwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Hivyo, kilimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura kuwaeleza wananchi wanaohusika na vitendo hivyo na Bunge liunde kamati maalum ya kuchunguza mauaji yote.

Kiongozi wa chama hicho, Dorooth Semu, ambaye alikuwapo hospitalini kutambua mwili, alisema anasikitishwa na ukimya wa Jeshi la Polisi kuwafichua watekelezaji wa matukio hayo.

Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, pia ametoa pole kwa CHADEMA kufuatia kifo cha kada huyo.

"Sisi vyama vya siasa linapokuja suala la ubinadamu siasa unaweka kando. Niombe Jeshi la Polisi litimize wajibu wake wa uchunguzi wa jambo hili," alisema Makalla.

Makalla alitoa pole hizo wakati akihutubia wananchi wa Wilaya ya Simanjiro katika eneo la Mirerani, ikiwa ni sehemu ya ziara yake mikoa ya Arusha na Manyara.

## HABARI KITAIFA

# Watuhumiwa mauaji mama, mwanawe wanaswa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya mama Mwamvita Mwakibasi (33) na mtoto wake Salma Ramadhan (12) nyumbani kwao, eneo la Mkonze, jijini Dodoma.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Alchelaus Mutalemwa aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Daudi Nyakungo (45), Rajab Rashid (45) na Fikiri Steven (40), wote wakazi wa Mkonze wanaohojiwa na uchunguzi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Kaimu Kamanda Mutalemwa alisema kuwa watu hao waliokuwa wakazi wa Mkonze, mtoto alikuwa mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mkonze, walifariki dunia wakiwa wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Walipigwa kitu butu kichwani wakiwa wamelala nyumbani kwao na kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji saa nane usiku Septemba 6, 2024," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu, pia kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi.

Juzi, miili yao wanafamilia hao ilisafirishwa kwenda Kiteto, mkoani Manyara kwa ajili ya maziko.

Akizungumza wakati wa kuaga miili hiyo, Diwani wa Mkonze, David Bochela aliwaomba wananchi wote kuwa watulivu na kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha mitaa yao inakuwa na usalama.

Mchungaji wa Kanisa la Assembly of God katika Mtaa wa Mkonze, Festo Mahinyila alitoa rai kwa serikali kuangalia kwa jicho la tatu nini kinaendelea katika jamii na sababu yake nini.

"Kwa upande wetu kama viongozi wa dini, tuchukue hatua ya kumrudia Mungu na kuwaita watu kumrudia Mungu, tufanye makongamano ya maombi ya kuomba toba na rehema kwa Mungu kwa kuwa ni vitendo ambavyo vinamchukiza Mungu wa mbinguni," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Waislamu nchini (Bakwata), Shekhe wa Kata ya Mkonze, Jumanne Kisaka, alisema tukio hilo linaonesha kukosa hofu ya Mungu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Coca-Cola Kwanza, Jonathan Jooste (katikati) akifurahia jambo na wafanyakazi wenzake wa Coca-Cola Tanzania, wakati wa uzinduzi wa tamasha la chakula la 'Coca-Cola Food Fest' ambalo linawaleta pamoja wapishi bora wa vyakula, muziki na burudani kama kumbukumbu ya urithi wa vyakula mbalimbali vya Tanzania. Uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Makalla: Wananchi waogopeni wanasiasa wenye uchonganishi

**Na Salome Kitomari,**
MONDULI

KATIBU wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, amewataka wananchi kuwaogopa na kuwakataa wanasiasa wanaopandikiza chuki kwa lengo la kuligawa taifa.

Makalla pia amewahakikishia Watanzania kuwa CCM kama chama kiongozi, itahakikisha uchaguzi ujao unakuwa huru na haki; atakayeshinda ndiye atakayetangazwa.

Akizungumza jana na wananchi wa Monduli katika eneo la Mto wa Mbu wakati wa mkutano wa hadhara, Makalla alisema ni muhimu wananchi wakaelewa kuwa maandamano hayajengi shule wala zahanati, bali ni kupoteza muda.

Alisema kuna wanasiasa wanaeneza chuki kuwa wafugaji watahamishwa na hawatakiwi nchini, jambo ambalo alisisitiza ni uongo ambao haupaswi kusikilizwa.

"Hatuna Tanzania nyingine, tusikubali kugombanishwa na watu ambao wana malengo yao, tutunze amani yetu kwa nguvu zote, Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wafugaji ndio maana ameleta miradi mingi ya maendeleo," alisema.

Makalla alisema lengo la ziara hiyo ni kuangalia uhai wa chama, kukagua utekelezaji Ilani ya CCM 2020-2025, kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika Daftari la Wakazi ili wawe na sifa ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Makalla alisema kuwa katika mikoa 17 waliyotembelea wamejiridhisha kuwa uhai wa chama uko vizuri na wana uhakika wa kushinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

"CCM haihitaji mbeleko, utekelezaji ilani yetu ni kielelezo tosha cha kurudi kwa wananchi... ukitembea kila mahali nchini kuna alama ya miradi ya maendeleo inayoachwa na Rais Samia, yote inawahusu wananchi, hivyo hatuhitaji kubebwabebwa bali tunajibeba wenyewe," alisema Makalla.

Katibu huyo alisema CCM kama chama kiongozi watahakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki na kwamba atakayeshinda kwa haki ndiye atakayetangazwa na si vinginevyo.

"Ni muhimu kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wanachagua viongozi wenyeviti wa vitongozi, kijiji, mitaa ambao ni muhimu sana. Matumaini tuliyonayo fedha za miradi zinapokuja zipate watekelezaji," alisema.

Alisema serikali imeshusha fedha nyingi za maji, zahanati, shule na kwamba ni muhimu watenge siku moja kati ya Septemba 11 hadi 20 mwaka huu 2024 kwenda kujiandikisha ili kupiga kura Novemba 27 mwaka huu.

"Wana CCM, mashabiki wa CCM, wasio na vyama ila wapenda maendeleo wajitokeze ili tumpe nguvu Rais Samia ambaye amethibitika ni mzalendo pekee anayeleta maendeleo, kila unapopita kuna alama ya mradi wa darasa, kituo cha afya, mradi wa maji, yote yamefanywa na serikali ya CCM," alisema.

Alisema ni muhimu vijiji 62 na vitongoji 230 viwe kijani (CCM), na kwamba chama hakitapitisha wagombea ambao watakilazimu kutumia dodoki na sabuni kuwasafisha.

"Mimi ndio msemaji wa chama, CCM itawaletea wagombea safi, wazuri wasio na makandokando kuja kufanya kazi nanyi, hatutaleta wagombea wanaoleta migogoro, wasiosoma taarifa za matumizi bali safi wanaostahili," alisema.

Alisema kuwa baadhi ya vyama vimekuwa vya matukio na havina wajibu wala dhamana kwa wananchi, bali CCM ndio yenye jukumu la kuleta maendeleo.

Alikosoa maandamano ya Chama cha Demokrasi na Maendeleo (CHADEMA), akidai hayajaleta maendeleo, bali yalikuwa ya kujidhururisha na kuwataka wananchi kutodanganyika.

"Wenzenu wanawaandamanisha wanapata posho, nyie mnaandamana bure na kuambiwa mkunje ngumi, CCM ina wajibu, ni chama kiongozi kitakachowaletea maendeleo," alisema.

Makalla alidai CHADEMA haina uwezo wa kushinda uchaguzi, bali inapotokea wameshinda ni kwa sababu kuna mgogoro ndani ya CCM.

Katika mkutano huo, Makalla alipokea kero 51 za wananchi 42, ikiwa ni pamoja na wananchi wawili kutoingizwa katika orodha ya wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) licha ya kuwa na sifa, ubovu wa barabara na shida ya maji

Pamela Ijumba Ofisa Kilimo Wilaya ya Monduli, akijibu baadhi ya kero, alisema kero ya mfereji kujaa matope itafanyiwa kazi baada ya uboreshaji skimu ya umwagiliaji, huku watendaji wengine wa serikali wakieleza mkakati wa kuzitatua kero zilizowasilishwa.

Baada ya ufafanuzi wa watendaji wa serikali, Makalla alisema CCM inawajibika na kero za wananchi na kwamba baada ya kupokea muhtasari wa namna kero za wananchi zitakavyotatuliwa kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, atawapigia mmoja baada ya mwingine kujua kama kero hizo zimetatuliwa.

HABARI KITAIFA

# Masauni ataka vyombo vya usalama kulinda amani wakati wa uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni (pichani) ameelekeza vyombo vya usalama vilivyopo chini ya wizara hiyo kujiandaa kwa uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Ameagiza vyombo hivyo kuacha milango wazi kwa wananchi wanaofika katika ofisi zao kutoa malalamiko mbalimbali.

Alitoa kauli hiyo mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki wakati anafunga semina elekezi kwa wakuu wa vyombo vya usalama, viongozi waandamizi na washiriki wa semina ambayo mada zake zililenga kuwajenga uwezo viongozi hao waandamizi, zikiwasilishwa na watoa mada kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

"Wizara hii ina vyombo ambavyo vimebeba taswira ya serikali, kwa maana nyingine vimebeba taswira ya wananchi. Hivyo, tukiwa tunatambua hayo na tukitembea na dhana ya R4, tutakwenda kubeba dhana hiyo hasa kipindi hiki ambacho tunaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu hapo mwakani.

"Kwahiyo, mjue kwamba wizara hii ni tegemeo kubwa sana na tuhakikishe tunaingia katika uchaguzi nchi yetu ikiendelea kubaki salama," alisema Masauni.

Waziri huyo pia alizungumzia suala la malalamiko ya wananchi, akitaka vyombo vya usalama vilivyopo chini ya wizara hiyo kuhakikisha kila mtu kwa nafasi yake ahakikishe anashughulikia malalamiko ya wananchi na kuyatafutia uvumbuzi na si kuacha wananchi wanazunguka na malalamiko yao.

"Suala la malalamiko hatuwezi kulifumbia macho, wananchi wengine ni wanyonge, maskini wanadhulumiwa, wananyanyasika kwa sababu hawana fedha na hawamjui mtu gani wa kumfuata wala hawana vyeo.

"Lazima tujue tuna dhima kubwa sana na tujaribu kujiweka katika nafasi zao hao watu, unakwenda sehemu husikilizwi, haki yako inapotea. Hivyo, ninatumai kwa kuwa leo mmeyafanya hayo hapa katika mafunzo, kila mtu kwa nafasi yake akirudi kituo cha kazi, atakwenda kutatua malalamiko ya wananchi na kwenye upungufu tukajirekebishe," aliagiza Masauni.



Akizungumza wakati wa ufungaji huo, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ally Gugu alieleza manufaa ya semina hiyo, mada 16 zikiwasilishwa na washiriki kupata muda wa kuuliza maswali huku Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Camillus Wambura akitoa neno la shukrani kwa niaba ya washiriki.

IPG Wambura pia alitoa ushuhuda wa faida za semina hiyo elekezi, akisema imewasaidia katika utendaji wao kuelekea katika utekelezaji wa majukumu yao.

# Wananchi 3,600 kulipwa bil. 46/- kupisha ushoroba

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi amezindua ulipaji fidia kwa wakazi 3,658 wanaohamishwa kutoka Kata ya Nyatwali, wilayani Bunda na kuwataka watumie fedha watakazolipwa kujiletea maendeleo.

Kanali Mtambi alizindua zoezi hilo mwishoni mwa wiki na kufafanua kuwa watalipwa Sh. bilioni 45.9 ili kupisha Hifadhi ya Serengeti.

"Wito wangu kwenu ni kwamba mtakapopata fedha zenu za fidia na kuondoka eneo hili, mkazitumie vizuri kwa maslahi ya familia zenu na kujiletea maendeleo," alisema Kanali Mtambi.

Aliwataka wanaume wasikimbilie kuwa na nyumba ndogo, bali watunze familia na kuweka mikakati ya pamoja namna ya kutumia fedha hizo.

"Eneo hili la Nyatwali ni mapito ya asili ya wanyamapori, pia linaweza kuwa na manufaa makubwa ya kiutalii hapa Bunda.

Hivyo, ni vyema mkaliona kama fursa za kiutalii ambazo baadaye zitawasaidia kama lilivyo eneo maarufu la Kogatende, Serengeti ambako nyumbu wanavuka," alisema.

Alifafanua kuwa serikali imetoa Sh. bilioni 45.9 za fidia huku fedha hizo zikiwa ni pamoja na nyongeza ya asilimia saba ambayo inatokana na ucheleweshwaji malipo tangu uthamini ulipofanyika.

Diwani wa Nyatwali, Malongo Mashimo alisema uzinduzi wa zoezi la malipo hayo ya fidia umemfanya awe na uhakika kuwa wakazi wa kata yake sasa watalipwa.

Mbunge wa Bunda Mjini, Robert Maboto, alisema wananchi wa Nyatwali wameelimishwa vizuri kuhusu fidia itakayotolewa na anaamini kila mmoja atapata haki yake.

"Shilingi bilioni 45.9 zimetengwa na serikali kwa ajili ya kuwalipa wananchi 3,658 wanaohamishwa kutoka eneo hili lenye ukubwa wa ekari 14,250.

"Serikali inachukua eneo hili kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi endelevu wa mfumo wa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na usalama wa wananchi," alisema Maboto.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA MARA, SIMIYU NA MANYARA (BABATI DC, HANANG DC, MBULU DC NA BABATI TC)

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa nne utafanyika katika Mikoa ya Mara, Simiyu, na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati tarehe 04 hadi 10 Septemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 04 hadi Jumanne tarehe 10 Septemba, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***
**Limetolewa tarehe 27 Agosti, 2024 na:**

Juma Rahisi.
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI



SHASHINHALE AUCTION MART & COURT BROCKERS LIMITED
(Dealers in: Court Broker, Debt Collectors, and Commission Agent, Legal consultant)
P.O BOX 288, GEITA. TANZANIA

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na Azania Bank,tutauza Midhana iliyowekwa, kwa njia ya Mnada kulingana na Tarehe zilizowekwa,

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNDA |
|---|---|---|---|
| 1 | KAYANDA NYALIKA | HOTEL ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE GEITA MJINI KIWANJ NA.13 KITALU "G" | 19/09/2024 |
| 2. | JOHNSON NICOLAUS MAHAGULA/JONHSON JACKSON NA PIUS CO LTD | NYUMBA YA MAKAZI IPO MTAA WA KAGERERA B,KIWANJA NA.244 KITALU "E" YENYE UMILIKI UNAOSOMEKA JONHSON NICOLAUS MAHAGULA | 20/09/2024 |
| 3. | GHATI JOSEPH CHACHA | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE,KIWANJA NA.169 NA 170 KITALU "C" GEITA MJINI | 19/09/2024 |
| 4. | PASCAL PETRO MUGABE/MILEM INVESTMENT CO LTD | NYUMBA YA BIASHARA KIWANJA NA.90 KITALU "E" E"GEITA MNJINI UMILIKI UNASOMA PASCAL PETRO MGABE.NYUMBA IPO KARIBU NA UWANJA WA KALANGALALA | 23/09/2024 |
| 5. | MARY LEONARD RUSHITA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE KIWANJA NA.132 KITALU "F" GEITA MJINI. | 23/09/2024 |
| 06 | ANDREW JOHN SHIRIMA/ANSI TIMBER GENERAL SUPPLIES LTD | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA NYAMALEMBO,KIWANJA NA.77 KITALU,GEITA MJINI YENYE UMILIKI UNAOSOMEKA ANDREW JOHN SHIRIMA. | 20/09/2024 |
| 07 | SAMWEL LUCAS MAGUHA | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO PASIANSI MWANZA KIWANJA NA.1114,KITALU "M" | 07/10/2024 |
| | | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO ILEMELA MWANZA KIWANJA NA.17 KITALU "A" | 08/10/2024 |
| | | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO KAHAMA MJINI KIWANJA NA.446 KITALU "A" | 30/09/2024 |
| | | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO IGUDIJA-KATA YA BUGHARAMA,WILAYA YA MSALALA. | 15/09/2024 |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atapaswa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada
3. Malipo ya 75% yanatakiwa kulipwa ndani ya siku 14,kushindwa kufanya hivyo 25% haitorudishwa.
4. Gharama za Kuhamisha umiliki,Kumwondoa aliepo ndani ya Nyumba Mdaiwa/Mpangaji zipo juu ya Mnunuzi.

**AU Azania Bank,**
**Mawasiliano Towers,Head Office,**
**S.l.p 32089 Dar es salaam,**
**255 222412025/6/7**

**Kwataarifa Zaidi wasiliana na,**
**Mkurugenzi Mtendaji,Shashinhale Auction Mart**
**Barabara ya Bomani Mahakamani, Geita Mjini**
**0657824547/0757006076.**

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

# WASILIANA NA KAMISHNA MKUU WA TRA KUPITIA SIKIKA APP

## Namna ya Kutumia

1. Ingia katika simu janja yako ya Android au IOS (Apple iphone au Ipad), kisha nenda sehemu ya kupakulia programu (Google play store au App Store) kisha tafuta programu ya 'TRA SIKIKA'.

2. Pakua 'TRA SIKIKA' kutoka Google Playstore kwa watumiaji wa simu za ANDROID, na kwa watumiaji wa simu za IOS (Apple Iphone au Ipad) pakua kutoka APP STORE.

3. Fungua 'SIKIKA APP' ambapo kurasa mbili za kwanza ni za kukukaribisha pamoja na ujumbe mfupi kutoka 'SIKIKA APP' (Welcome Message / App Intro).

4. 'SIKIKA APP' inakuwezesha kutuma maoni au malalamiko pamoja na kuyafuatilia.

5. Kutuma maoni bonyeza kitufe cha maoni , kisha andika maoni yako na bonyeza kitufe cha wasilisha. Utapata ujumbe wa maoni yako kupokelewa pamoja na Namba ya Kufuatilia (Track Number).

6. Kutuma malalamiko bonyeza kitufe cha malalamiko , kisha andika malalamiko yako na bonyeza kitufe cha wasilisha. Utapata ujumbe wa kupokelewa kwa malalamiko yako pamoja na namba ya kufuatilia (Track Number).

7. Kufuatilia maoni au malalamiko bonyeza kitufe cha fuatilia kisha ingiza namba uliyopewa baada ya kutuma maoni au malalamiko kisha bonyeza kitufe cha tuma. (Utapokea Ujumbe kuhusu utekelezaji wa Maoni au Malamiko yako).

TRA

## TRA SIKIKA APP



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF wamulikeni wachambuzi redio, TV wanaharibu soka

**KUNA** wimbi kubwa la wachambuzi wa michezo hasa kwenye redio na televisheni nchini Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni.

Asilimia kubwa wanachambua soka tu na si michezo mingine na wanafanya hivyo huku wakiwa hawana taaluma hiyo na kutokuwa na ufahamu wa kutosha katika mchezo huo unaopendwa na watu wengi, wakionekana wazi ni kama tu kutumia vipaza sauti hivyo kujipatia umaarufu.

Kinachoonekana ni kwamba wengi wao hawana hata ufahamu wa soka lenyewe, bali wamekuja au kuletwa ili tu kujipatia mkate wao wa siku.

Vipindi vya michezo kwa sasa vinaonekana ni vya kupiga soga zaidi, kubishana, kutengeneza ajenda zenye kuleta taharuki kwa mashabiki kwa sababu ya faida ya watu fulani ambao wapo nje ya redio na televisheni zao.

Ukiwasikiliza wanavyoongea ni kama vile wanakuwa na chuki, au kutumwa kuziandana baadhi ya klabu, wachezaji na viongozi wa klabu fulani.

Kuna wakati unaweza kuona kama ajenda zimetengenezwa makusudi kwani mada hiyo hiyo inakuwa kwenye redio mbili au tatu, na wote wanaongea kilekile, ikionekana kana kwamba mpango huo umetengenezwa mahsusi, jambo ambalo tunaona ni hatari kwa soka letu ambalo linapiga hatua kila uchao.

Wachambuzi siku hizi hawachambui mpira kama msingi wa kazi yao iliyowapeleka studio, badala yake wamekuwa wakichambua kila kitu.

Wanachambua mikataba ya wachezaji, udhamini wa klabu kama ni halali au si halali, unastahili ama la, wanahoji uhalali wa kubalisha nembo ya klabu, uwekezaji na vitu vingine ambavyo ilibidi waalikwe au watafutwe watu wenye taaluma na vitu hivyo.

Wachambuzi sasa hivi wanaweza hata wakachambua kuwa mchezaji ni halali kusajili timu fulani na si fulani kihisia tu na si matakwa na mahitaji ya timu husika.

Cha kushangaza ni hata soka lenyewe wamekuwa wakichambua kishabiki mno, na ukitaka kujua hilo, mchezaji mpya wa Klabu A anapewa muda, lakini wa Klabu B, anaambiwa amefeli, wakati wote wamecheza mechi moja, hapo tunajiuliza ni nani aliyesimama nyuma ya wachambuzi hawa?.

Wachambuzi wanakwenda mbali zaidi mpaka wanachambua aina ya utambulisho wa wachezaji klabu gani imetambulisha vizuri, au jezi za klabu gani nzuri kuliko za timu nyingine.

Hao ndio aina ya baadhi ya wachambuzi waliopo nchini ambao wamebahatika kupata nafasi adimu ya kutumia vyombo hivyo vya habari kuelimisha wanamichezo lakini baadhi wamekuwa wakitumia jukwaa hilo kuharibu kabisa soka la nchini hii ambalo limekuwa kivutio kikubwa cha wageni kuja kucheza na kufundisha.


Kwa namna mwendo ulivyo sasa Nipashe tunashauri ufike wakati sasa wachambuzi wawe wanajitambulisha kwanza kama ni mashabiki wa klabu gani (declare interest), kama wanavyofanya wale wa nje, ili mashabiki wawaelewe badala ya kujificha kwenye kivuli cha uchambuzi kumbe wana ajenda zao kama si maslahi fulani.

Tunachokiona hapa Shirikisho la Soka nchini (TFF), linapaswa kutupa jicho la ziada upande huo hata kwa kuomba ushirikiano kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ambyo imejidhatiti kutoa huduma bora kwa wateja na wadau wake wote, ili kuona namna ya kudhibiti wimbi hili la wachambuzi uchwara katika soka.

Nipashe tulitegemea kuona wachambuzi wa michezo wakifanya kazi ya kuwaelimisha mashabiki ambao wengi huwaamini kuwa wanajua vitu vingini, lakini badala yake wao ndiyo wanazidisha taharuki zaidi na kuharibu soka la Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuzitumia Simba, Yanga kuitengeneza Stars ni uwezo wa mwisho wa kufikiri

**BADO** baadhi ya mashabiki wa soka na wachambuzi wana mawazo 'mgando' yale yale kuwa, uwapo wa wachezaji wa kigeni nchini wanasababisha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, isiwe bora.

Hivi karibuni, kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu, Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia, alilikemea suala hili akisema si kweli, badala yake limesaidia sana kuimarisha kikosi cha Taifa Stars, jambo ambalo bega kwa bega naungana naye, na kongole kubwa kwake.

Karia akasema ukihesabu idadi ya wachezaji wa kigeni waliopo nchini ni wachache sana ukilinganisha na wazawa, hivyo akapinga kabisa mawazo kuwa wanazuia nafasi za wazawa kuonesha vipaji vyao ili waonekane kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Kikubwa zaidi akawataka wachezaji wa Kitanzania ambao wanaona kama wanabanwa sana, kutoka ndani ya nchi, kusaka malisho mengine nje ambako wataona watapata nafasi za kucheza.

Pamoja na Rais Karia kuongea hivyo, bado kuna watu wameendelea kuamini vile vile kuwa wageni wamekuwa wengi kwenye ligi ya Tanzania na kutaka wapunguzwe.

Kibaya zaidi mjadala hivi sasa umehamia pia kwa makipa, wahafidhina wakidai iwekwe kanuni ya kutokuwapo makipa ya kigeni nchini kwani unawafanya makipa wa Tanzania kukosa nafasi kwenye klabu zao, hivyo Stars kuchukua ambao hawapati nafasi kwenye vikosi vya Simba na Yanga.

> **Kibaya zaidi mjadala hivi sasa umehamia pia kwa makipa, wahafidhina wakidai iwekwe kanuni ya kutokuwapo makipa ya kigeni nchini kwani unawafanya makipa wa Tanzania kukosa nafasi kwenye klabu zao, hivyo Stars kuchukua ambao hawapati nafasi kwenye vikosi vya Simba na Yanga.**

Ali Salim wa Simba na Aboutwalib Mshery wa Yanga ni makipa wa Stars ambao hawapati nafasi za kuanza kwenye vikosi vyao kutokana na uwapo wa Moussa Camara na Djigui Diarra.

Mawazo haya ni ya kuzikosea heshima Klabu za Simba na Yanga ambazo mipango na malengo yao ni kushindana kwenye michuano ya kimataifa na ikiwezekana kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, na si kuwa akademi ya Taifa Stars.

Kutengeneza kanuni ili makipa hao wawe namba moja kwenye vikosi vya Simba na Yanga ni mawazo mfu, kwani kipa yeyote mzuri anawekwa langoni kwa juhudi na uwezo wake na wala si kanuni.

Hakuna kocha yeyote kati ya Fadlu Davids wa Simba na Miguel Gamondi wa Yanga anaweza kumpanga mchezaji kwa sababu ya utaifa wake badala ya kuangalia uwezo.

Ifikie mahali Watanzania tuangalie zaidi tulipojikwa na si tulipoangukia. Suala ya kutoka suluhu dhidi ya Ethiopia lisitutoe mchezoni, pia uwezo wa wachezaji wa Kitanzania ni suala mtambuka na si la mtu mmoja.

Ni aibu kwa Tanzania kutaka kuwekwa sheria na kanuni nyingi za kibaguzi, wakati kuna nchi hapa hapa Afrika ambazo zinateua wachezaji wa timu ya taifa wote kutoka nje ya nchi.

Nchi jirani tu kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambayo haina kikomo cha wachezaji wa kigeni kwenye ligi yao, ndiyo maana TP Mazembe inajaza robo tatu ya wageni, lakini ikiita timu ya taifa wengi wanatoka nje ya nchi na ni imara zaidi, ikiwa ni moja kati ya timu tishio Afrika.

Nadhani kama taifa tungeanza kuangalia wenzetu, nchi ambayo haijatulia hata kwa amani, lakini ina wachezaji wengi wenye vipaji halisi ambavyo havina haja ya kuvilinda hata kwa kanuni.

Tujiulize tu kama Maxi Nzengeli haijaitwa kwenye kikosi cha DR Congo, au Pacome Zouzoa na Jean Charles Ahoua hawajaitwa kikosi cha Ivory Coast, wenzetu wana aina gani ya wachezaji?

Je, hawa wangekuwa Watanzania wasingekuwapo Stars? Je, Stars ina aina hiyo ya wachezaji? Hapa ndipo unapopata majibu kwa nini Simba na Yanga zinakwenda kusajili wachezaji nje. Na pia inaonesha kuwa kama nchi kuna sehemu tunakosa kwenye kuzalisha vipaji vya wachezaji. Tuanzie hapo, siyo kuzuia wageni na kuweka kanuni zisizo na kichwa wala miguu.

# GGML kusaidia Tanzania kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Uchimbaji Madini ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imesisitiza dhamira yake ya kuendelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine kuhakikisha Tanzania inapiga hatua katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG) ifikapo mwaka 2030.

Dhamira hiyo ya GGML imewekwa wazi na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Stephen Mhando kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo wakati hafla ya utoaji tuzo maalum za utambuzi wa biashara na mashirika ambayo yanaongoza katika kuendeleza malengo ya SDG na kuleta matokeo chanya kwa jamii na mazingira.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo zilizoandaliwa na Mtandao wa Kimataifa wa Compact Tanzania (GCNT), ilifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam huku GGML ikinyakua tuzo mbili, ikiwa ni ishara ya utambuzi wa kampuni hiyo katika kutekeleza na kufanikisha ufikiwaji malengo hayo ya maendeleo endelevu.

"Kwa kutambua umuhimu wa malengo ya SDG, GGML pamoja na kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza mambo yote muhimu kwenye malengo haya, tumeendelea kudhamini utoaji tuzo hizo ili kutambua na kusherehekea mchango wa Watanzania katika kufikia malengo hayo endelevu," alisema Mhando.

Kwa mujibu wa Mhando, malengo hayo ya SDG yanawiana na maadili ya mpango kazi wa GGML ambao unalenga uendelevu, ubora na ushirikiano.

"Hii ni moja ya sababu muhimu GGML tumetoa mchango wa maana katika kufanikisha malengo kadhaa muhimu ya SDG, likiwamo lengo namba sita linalohusu maji safi na usafi wa mazingira ambapo kupitia miradi kama ya maji wa Geita, GGML tumewekeza dola za Marekani milioni sita ili kufikisha maji safi kwa zaidi ya wakazi 150,000 wa Mkoa wa Geita na kuboresha upatikanaji maji safi kwa asilimia 70 mkoani humo," alisema.

Alisema kampuni hiyo imetekeleza lengo namba nane la SDG ambalo linahusu kazi zenye staha pamoja na ukuaji uchumi kwa kutoa maelfu ya ajira, kusaidia biashara za ndani na kuchangia maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

"Lengo namba nne la SDG ambalo linalozungumzia elimu bora, GGML imewekeza katika ujenzi wa shule na kuibua programu za elimu zinazowezesha kizazi kijacho cha viongozi.

"SDG 13 ambalo linazungumzia namna ya kuchukua hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, kwa upande wa GGML imehakikisha kwamba shughuli zake zinakidhi viwango vya juu zaidi vya mazingira na kwa kuwekeza katika teknolojia endelevu zinazoboresha uhifadhi wa kama vile uzinduzi wa hivi karibuni wa Kituo Kidogo cha 33/11KV ambacho ni alama ya kipekee kwa kampuni kuanza kutumia umeme wa Gridi ya Taifa unaotolewa na TANESCO," alisema.

Akizungumzia tuzo hizo, ofisa huyo alisema zinaashiria zaidi ya uwajibikaji wa shirika kwa kuwa zinatambua kazi kubwa inayofanywa na mashirika yote Tanzania kuelekea mustakabali endelevu.

"Tunapoherehekea mafanikio haya tunalenga kuthibitisha dhamira yetu ya kufanya kazi bega kwa bega na wadau wote ili kuhakikisha hatumwachi mtu nyuma katika safari hii ya kuelekea maendeleo endelevu.

"Ni kwa sababu hii kampuni ya GGML ambayo ni kampuni tanzu ya AngloGold Ashanti tunaunga mkono Kanuni za Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, kazi, mazingira na mapambano dhidi ya rushwa," alisema.

Kwa mujibu wa Mhando, Julai 2024 kampuni hiyo ilithibitisha upya nia hiyo kupitia maombi yake kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kujiunga rasmi na Mkataba wa Kimataifa wa Umoja huo kupitia Mtandao wa Global Compact Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Katibu Mtendaji - Biashara na Ubunifu kutoka Tume ya Mipango, Dk. Lorah Madete alipongeza uazishwaji tuzo hizo na kueleza kuwa zimekuwa chachu katika kuwezesha Tanzania pamoja na kampuni mbalimbali nchini kutambua namna zinavyopiga hatua kufikia malengo hayo ya maendeleo endelevu.



Mtaalamu wa masuala ya jinsia, Regina Kabwogi akiwasilisha mada ya jinsia kuhusu migongano ya binadamu na wanyamapori kwenye kongamano kwa wahariri lililoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira wilayani Bagamoyo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri Mkuu: Tumeongeza wigo huduma za watoto wachanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali imefanya mageuzi makubwa kwa kuongeza wigo wa upatikanaji huduma kwa watoto wachanga.

"Serikali imekuwa inatekeleza mikakati na afua mahsusi za kuhakikisha upatikanaji huduma bora kwa watoto wachanga. Ni jambo la fahari sana kuwa hivi sasa huduma maalum za watoto wachanga na ile ya Mama Kangaroo hadi kufikia Julai 2024, zimeanzishwa katika hospitali 245," amesema.

Majaliwa aliyasema hayo juzi wakati anazungumza na viongozi na wadau walioshiriki mbio za hisani za 2024 zilizoandaliwa na Benki ya Maendeleo (Maendeleo Bank Marathon 2024) katika viwanja vya Green Park, Oysterbay, jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu alisema mafanikio hayo yametokana na dhamira ya dhati ya serikali kuhakikisha Tanzania inapunguza vifo vya watoto wachanga kufikia lengo namba tatu la Maendeleo Endelevu la vifo chini ya 12 katika kila vizazi hai 1,000 kufikia mwaka 2030 kutoka vifo 24 kwa kila vizazi hai 1,000 kwa mwaka 2022.

Akizungumzia kuhusu kaulimbiu ya tukio hilo ambayo ni Hatua ya Faraja - Msimu wa Pili, Waziri Mkuu alisema inasawiri mpango wa benki hiyo wa kuendeleza kazi yao ya mwaka jana ya ununuzi wa vitanda maalum vya kutunzia watoto njiti (Infant Baby Warmer) katika Hospitali ya KCMC na ujenzi wa kituo kipya cha watoto wenye changamoto ya ulemavu wa akili na usonji kinachotarajiwa kujengwa wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

"Kama mlivyosikia, pale KCMC idadi ya vifo vya watoto wanaozaliwa njiti ni kubwa na ipo kati ya asilimia 20 mpaka 25. Hawa ni binadamu wenzetu wanaostahili kuishi na tuna kila sababu ya kuonesha upendo kwa kuchangia hatua za faraja.

"Hivyo basi, nitoe wito kwa wananchi wote wenye mapenzi mema kuendelea kuiunga mkono Benki ya Maendeleo katika utekelezaji afua hizi muhimu," alisisitiza.

Aliwapongeza viongozi wa benki hiyo kwa kuongeza lengo la uchangiaji kwenye mbio za mwaka huu kutoka Sh. milioni 120 hadi Sh. milioni 200 ili kukamilisha kazi waliyoianza mwaka jana.

Kuhusu mchango wa madhehebu ya dini, Waziri Mkuu alisema serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa wadau wa sekta binafsi katika kutoa huduma za jamii, zikiwamo zinazohusu sekta za afya, elimu, maji na nyinginezo.

"Ninawapongeza sana Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kwa kutoa eneo kubwa zaidi kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha watoto wenye changamoto ya ulemavu wa akili na usonji.

"Nimeelezwa kuwa kituo hicho kitajengwa eneo la Kitopeni, wilayani Bagamoyo ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii," Waziri Mkuu alipongeza.

Aliwapongeza viongozi wa Benki ya Maendeleo kwa kufanikiwa kuongeza hadhi ya leseni ya uendeshaji kutoka kuwa Benki ya Kanda (Community Bank) na kupandishwa hadhi ya kuwa Benki ya Biashara ya Kitaifa (Fully-fledged Commercial Bank) kwa kuwa hatua hiyo inawaruhusu kufungua matawi nchi nzima.

"Pia ninawapongeza sana kwa ubunifu kwa kuanzisha huduma mbalimbali kama vile mikopo ya nishati mbadala, mikopo ya rasimisha ardhi, mikopo ya bajaji na bodaboda kwa vijana na mikopo ya biashara kwa machinga (Wezesha Machinga).

"Nimeambiwa kwa kushirikiana na uongozi wa machinga, mmebuni mradi wa MACHINGA HOUSE- SAMIA CITY unaojumuisha zaidi ya viwanja 500 na zaidi ya ekari 90 katika Kijiji cha Magoza, kilichoko Bagamoyo ambako zaidi ya machinga 500 watanufaika na mikopo hiyo katika awamu ya kwanza," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisema serikali imeendelea kusaidia Hospitali ya KCMC kwa kuipatia fedha za dawa na vifaa tiba.

"Katika ziara yake, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alikwenda kuzindua jengo la kansa na akaelekeza Sh. bilioni tano zipelekwe kwenye hospitali hiyo.

"Hadi sasa, Sh. bilioni tatu zimeshatolewa, Sh. bilioni moja zitatumwa ndani wiki mbili zijazo na Sh. bilioni moja iliyobakia itatumwa kabla ya Januari 2025.


"Pia magari mawili mapya ya kubebea wagonjwa, yataletwa kabla ya Oktoba mwaka huu," alisema Naibu Waziri Mollel.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Maendeleo Bank, Peter Tarimo, alisema msukumo wao wa kurudi kusaidia Kituo cha Mtoni Diakonia umetokana na uhitaji mkubwa uliopo ambapo kwa sasa kina watoto 107 kutoka pande zote za Tanzania Bara na Zanzibar ambao wanafundishwa kituoni huko.

"Watoto wengine 86 wanafikiwa majumbani kwao kupitia programu ya elimu ya majumbani na wengine 80 wamekosa nafasi ya kujiunga kutokana na uhaba wa miundombinu, yakiwamo madarasa na mabweni," alisema.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Kituo cha huduma za kisheria chazinduliwa

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Katiba na Sheria imezindua rasmi Kituo cha Huduma kwa Mteja cha Huduma za Kisheria ambacho kitakuwa kinapokea malalamiko, hoja, maswali na tuhuma za rushwa kwa njia ya simu kutoka kwa wananchi na kutatuliwa moja kwa moja na wataalamu.

Kituo hicho kilizinduliwa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma na Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (pichani) kama sehemu ya Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Prof. Kabudi alisema wizara imeanzisha kituo hicho baada ya kubaini malalamiko mengi ya wananchi yamekuwa yanawasilishwa wizarani kwa njia ya barua au kufika moja kwa moja kwenye ofisi za wizara kwa kutumia gharama kubwa za usafiri na kujikimu wakiwa Dodoma.



Alisema kupitia huduma hiyo, wananchi walioko maeneo ya mbali hivi sasa watakuwa wanawasilisha malalamiko yao kwa njia ya simu katika kituo hicho na yakafanyiwa kazi kwa wakati bila kulazimika kufika ofisi za wizara.

"Kituo hiki ni ishara ya maendeleo na udhibitisho wa dhamana ya kuwahudumia Watanzania kwa bidii, uwazi na uadilifu.

Ni hatua muhimu inayohitajika katika kuboresha njia za serikali za kushirikiana katika utoaji huduma.

"Juhudi hizi ni muhimu kwa kuwa wananchi wanakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo kituo hiki ni ishara ya wazi ya serikali kutumia njia rahisi za kiteknolojia kuwafikia wananchi ili wawasilishe changamoto zao na kutatuliwa kwa ufanisi na kwa wakati.

"Kituo kinafanya kazi saa zote za kazi na wizara inafikiria kuongeza muda kifanye kazi kwa saa 24 siku zote saba za wiki," alisema Prof. Kabudi.

Mkurugenzi wa Katiba na Ufuatiliaji Haki Wizara ya Katiba na Sheria, Jane Lyimo, alisema malengo la kuanzisha kituo hicho ni pamoja na kuboresha mifumo ya mawasiliano na huduma kwa umma.

Vilevile, kituo hicho alisema ni matokeo ya programu ya kujenga taasisi katika kupambana na rushwa inayotekelezwa na wizara hiyo kwa lengo maalum la kuziwezesha taasisi ikiwamo wizara katika kupambana na rushwa nchini.


"Tunashukuru sana uanzishwaji kituo cha huduma kwa mteja cha huduma za kisheria kwa ajili ya kupokea taarifa na malalamiko yanayohusu tuhuma za rushwa, ukiukwaji haki unaofanywa na taasisi au mtu mmoja mmoja na maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi kuhusiana na huduma zinazotolewa na wizara ya katiba na sheria pamoja na taasisi zote zilizo katika mnyororo wa haki.

Hii itarahisisha kutatua kwa haraka shida za wananchi," alisema Jane.

Alisema serikali iliamua kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja ambapo mwananchi anaweza kuwasilisha malalamiko yake kupitia namba ya simu 026216036 na kwamba huduma hiyo inasaidia kufikia wananchi wengi hususani wasio na uwezo wa kumudu gharama za usafiri kwenda kuwasilisha malalamiko yao wizarani.

"Kupitia kituo hiki, Wizara ya Katiba na Sheria imejipanga kutoa huduma bora kwa wananchi tukitambua kwamba mawasiliano ya haraka, sahihi, muhimu katika kuhakikisha usawa, uwazi na haki katika jamii yetu, hivyo tunajiweka wazi kusikiliza maswali na malalamiko yote ya wananchi kwa kutolewa kwa njia bora zaidi," alisema Jane.

Aliomba wadau mbalimbali, ikiwamo taasisi za serikali, kuendelea kushirikiana na wizara katika kuhakikisha hoja, malalamiko yote, maswali kama yanagusa taasisi husika yatatuliwe ili kurahisisha mchakato wa kumhudumia mwananchi kupitia kituo hicho uende kwa kasi na ufanisi.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. ................ OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

GEOFREY KUNDY..........................................ACCUSED PERSON

To:
Geofrey Kundy
Kilongawima Area, Mbezi Beach
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13 day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name..........................................

Signature.....................................

Qualification/Relationship

Date...........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. 19337 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

ERICO ELIEZA MGENI..........................................ACCUSED PERSON

To:
Erico Elieza Mgeni
Manzese Area, Ubungo Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13 day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name..........................................

Signature.....................................

Qualification/Relationship

Date...........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KISUTU)

CRIMINAL CASE NO. 19328 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

FLAVIANUS MOMBA MAHITI..........................................ACCUSED PERSON

To:
Flavianus Momba Mahiti
Plot No. 28945, Kinyerezi Area,
Ilala Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 18th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name..........................................

Signature.....................................

Qualification/Relationship

Date...........................................



Askari polisi wa mkoa wa Manyara, wakishiriki mazoezi mjini Babati juzi ikiwa ni shamrashamra ya kuelekea kilele cha miaka 60 ya jeshi la polisi. **PICHA: GIFT THADEY**

# BAKWATA yalaani ubakaji, ulawiti kwa watoto

**Na Steven William,** MUHEZA

BARAZA Kuu la Waislam Mkoa wa Tanga (BAKWATA), limelaani vitendo vya ubakaji na ulawiti kwa watoto ambao umekithiri katika jamii, huku likiitaka serikali kuchukua hatua kali kwa wahusika.

Shehe Mkuu wa BAKWATA mkoani hapa, Ally Luwuchu, alitoa kalipio hilo wakati akizungumza na waislamu katika dua ya familia ya marehemu Shehe Juma Rashid Semkati iliyofanyika Kijiji cha Kibanda, Wilaya ya Muheza.

Alisema amefanya utafiti mdogo mkoani Tanga na kugundua uwepo wa wimbi kubwa la matukio ya ubakaji na ulawiti kwa watoto chini ya umri wa miaka 18.

"Matukio haya ni ya kikatili na aibu kubwa, hayavumiliki katika jamii na jambo hili linakemewa vikali hata katika mihimili ya dola nchini ikiwemo Bunge, serikali na mahakama, hivyo kila mmoja katika jamii anawajibika kumlinda mtoto mahali kokote anapokuwa," alisema shekhe huyo.

Alisema kuwa ikibainika mtu yeyote ametenda kosa la namna hiyo apate adhabu kubwa inayoanzia kifungo cha miaka 30 au kifungo cha maisha jela ili iwe fundisho.

Pia aliwaasa waislamu na wananchi wote kujiepusha na vitendo hivyo ili kuwalinda watoto na kutotumbukia kwenye madhira ya kukumbana na adhabu kali zinazotolewa na mahakama kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**Alisema kuwa ili kulinda maadili ya watoto lazima wajengewe maadili ikiwamo kumcha Mungu kwa kuwapelekea kusoma elimu ya madrasa.**

Msimamizi wa shughuli hiyo, Kapteni Mohamed Kaboyo alisema kuwa wazazi wanajukumu la kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia. Alisema kuwa ili kulinda maadili ya watoto lazima wajengewe maadili ikiwamo kumcha Mungu kwa kuwapelekea kusoma elimu ya madrasa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kisutu Dar es Salaam, Chiku Mhando alisema wanafunzi wanaosoma masomo ya dini wanapata uwelewa wa kumjua Mungu na kuwa na maadili mema.

Baadhi ya waumini wa dini ya kiislam wilayani Muheza, Makame Seif, Mauld Meta, Cheche Abdallah na Said Kitomondo kwa nyakati tofauti walisema kuwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto vinasikitisha na kuiomba serikali kuchukua hatua kali kwa whusika iwe fundisho.

Katika shughuli hiyo familia ya shekhe Jumaa Rashid Semkati walitoa zawadi ya misahafu zaidi ya 100 kupeleka katika msikiti mbalimbali na shule za sekondari. Msemaji wa shughuli hiyo, Jumanne Mhando, alisema kuwa lengo la shughuli hiyo ilikuwa kusoma dua ya familia ya shekhe Juma Rashid Semkati pamoja na dua ya kuombea jamii na nchi.

# Wanawake watakaogombea uongozi kujengewa uwezo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAWAKE 72 watakaoonesha nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwenye kata sita za Moshi Vijijini na Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, watajengewa uwezo wa kukabiliana na unyanyasaji wa kingono.

Mpango wa kuwainua wanawake kisiasa uko chini ya utekelezaji wa 'Mradi wa Sauti ya Haki' unaolenga kuendeleza majukwaa ya wanawake, kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea uchaguzi huo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mjini hapa, Mratibu wa mradi huo wa miezi sita unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT), Veronica Ollomi alisema wanawake hao ni kati ya watu 100 waliolengwa kujengewa uwezo katika masuala ya uongozi.

"Tunajua katika mchakato kama uchaguzi kuna rushwa ya ngono na rushwa mbalimbali. Je? yeye kama mwanamke anayetamani kuwa kiongozi akabiliane vipi na hizo changamoto ambazo zinaweza zikajitokeza katika mchakato mzima wa kugombea hizo nafasi za uongozi" alihoji.

Alisema idadi ambayo wataifikia katika kata zote sita ni watu 100, lakini katika hao, 72 ni wanawake na 28 ni wanaume, kwamba wameweka kundi la wanaume kwa sababu ni chachu ya mabadiliko.

Alisema mradi huo unalenga zaidi kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi, kwa kuwa suala la ushiriki kwenye mchakato wa uchaguzi ni haki ya msingi ya binadamu.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika Kata ya Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi) na Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

Ollomi alisema: "Walengwa wetu ambao tutakuwa nao katika harakati hizi ni pamoja na wanaharakati wanawake ambao ni vikundi tulivyoviunda kipindi kilichopita kutoka kwenye hizo kata"

Mrakibu wa Polisi (SP), Asia Matauka, ambaye ni Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, alisema itakapotokea changamoto ya kisheria polisi dawati ndipo inapohusika moja kwa moja

# Makinda azindua mafunzo ya wasimamizi PSSNII

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SPIKA Mstaafu wa Bunge na Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Anne Makinda, amezindua mafunzo ya wasimamizi na wadadisi watakaofanya utafiti wa mwisho wa kutathimini Mpango wa Pili wa Kunusuru Kaya Masikini Tanzania wa Mwaka 2024/2025 (PSSN II).

Akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa uzinduzi huo uliowahusisha wataalamu hao 135, Makinda alisema mikoa 17 (14 Bara na 3 Zanzibar), vijiji/mitaa/shehia 434 zitatembelewa, kwamba kati ya hivyo vijiji/mitaa 376 ni kutoka Tanzania Bara na shehia 58 ni kutoka Zanzibar.

Alisema utafiti huo utafanyika chini ya Ofisi ya Taifa yaTakwimu (NBS).

"Serikali inatekeleza zoezi hili la kufanya tathmini ili kuweza kupima endapo mpangohuu unafikia malengo yaliyokusudiwa ya kuondoa umaskini kwa kaya zilizoainishwa kuishi katika umaskini uliokithiri. Tathmini kama hii pia hufanyika katika nchi mbalimbali zinazotekeleza mpango kama huu duniani kupitia taasisi za fedha na maendeleo za kimataifa,"alisema Makinda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Shedrack Mziray, alisema katika kusaidia kutatua changamoto za upungufu wa miundombinu ya huduma za jamii na ajira kwa wananchi na umaskini wa kipato kwa walengwa, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Nchi zinazozalisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OFID), umetoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi 1,518 ya kuendeleza miundombinu.

Alisema fedha hizo zitasaidia kutoa ajira za muda na kuza uchumi wa kaya. Aliitaja miradi hiyo ni ya sekta za afya, barabara, elimu, maji, kilimo, ufugaji na mazingira.

Mziray alisema hadi kufikia Juni 2024, zaidi ya asilimia 51.3 ya miradi hiyo ilikuwa imekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi, kwamba imegharimu zaidi ya Sh. bilioni 82.

Alisema: "Ili kukuza uchumi wa kaya, ambao unahusisha uhamasishaji wa kuunda vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya kuongeza kipato, kufikia Juni mwaka huu, kulikuwa na vikundi 60,342 vyenye wanachama 838,241. Kati ya wanachama hao, wanawake ni 716,515 (84.5%) na wanaume ni 121,726 (14.5%).

Alisema vikundi hivyo vimekusanya akiba ya Sh. bilioni 7.9 na kukopeshana Sh. bilioni 3.2 kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi inayowaongezea kipato.

Vilevile alisema kaya za walengwa 84,674 wamepewa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara na kupatiwa ruzuku ya kuanzisha shughuli za kiuchumi yenye thamani ya Sh.bilioni 31.3 hadi kufikia Juni 2024.

Hadi kufikia Juni 2024, kaya 394,500 yenye wastani wa watu 1,893,600 zili-





# CHADEMA, CCM waungana kuhimiza maboresho daftari

**Na Samson Chacha,**
TARIME

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Tarime mkoani Mara, wameungana kuhimiza wananchi wenye sifa kushiriki kikamilifu katika maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, huku wakisisitiza umakini katika kuwabaini raia kutoka nje.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kufuatia mchakato huo ulioanza Septemba 4, walisema hatua hiyo itasaidia kuongeza wapiga kura wapya, ikiwamo kuwapa fursa wananchi wote wilayani humo kuwa na sifa pamoja na vigezo vya kuchagua viongozi wanaowahitaji.

Diwani wa Kata ya Sirari (CCM), Amos Sagara alisema wanahakikisha wanahimiza wananchi wenye sifa, huku akiwataka maofisa uandikishaji kuwa makini na wahamiaji kujipenyeza na kujiandikisha bila kufuata utaratibu.

**Diwani wa Kata ya Sirari (CCM), Amos Sagara alisema wanahakikisha wanahimiza wananchi wenye sifa, huku akiwataka maofisa uandikishaji kuwa makini na wahamiaji kujipenyeza...**

Mwenyekiti wa CHADEMA Tarime Mjini, Bashir Abdalah alisema majimbo ya Tarime Mjini na Tarime Vijijini wanaendelea kuhimiza vijana, kinamama na wazee kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili kuleta mabadiliko.

Mwenyekiti wa CHADEMA Tarime Vijijini, Mwita Sasi alisema: "Tunawahimiza mawakala wetu na wa vyama vingine ambao wameteuliwa kusimamia katika zoezi hili la kuwa makini na uadilifu kwa kuwatambua wakazi halali wa maeneo yao ili kuepuka watu wajanja watakao kuwa na nia ovu inayoweza kuleta migogoro kisiasa".




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (wa pili kulia) na viongozi wengine, wakiwa na mfano wa cheki mwishoni mwa wiki, alipofika Kata ya Nyatwali wilayani Bunda kuzindua zoezi la ulipaji wa fidia kwa wakazi kata hiyo ili wapishe eneo kwa ajili Hifadhi ya Serengeti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjumbe CCM achangia mifuko 100 ya saruji

**Na Mwandishi Wetu,**
MARA

MJUMBE wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kutokea Wilaya ya Rorya, Sango Kasera amekabidhi mifuko 100 ya saruji kwa ajili kuunga mkono ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa chama hicho.

Hatua ya kukabidhiwa msaada huo inakifanya CCM Mkoa wa Mara, kuendelea na mchakato wake wa kuhakikisha inakuwa na ukumbi wa kisasa wa mikutano.

Akikabidhi mifuko hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 2.3 kwa Katibu wa CCM Mkoa wa Mara, Mjanael Mjanael kwa niaba ya Mjumbe wa Mkutao Mkuu wa Taifa, Mbunge Mstaafu wa Rorya Lameck Airo, alisema kuwa ametumwa kukabidhi mifuko hiyo kwa kuwa wana CCM wana wajibu wa kukijenga chama chao.

"Ninaomba nikabidhi mifUko hii ya saruji 100 yenye thamani ya Sh. milioni 2.3 kwa niaba ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, Sango Kasera kwa ajili ya kuunga mkono uamuzi wa chama katika kuhakikisha kila mwanachama anawajibu wa kukijenga chama," alisema.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mara, Mjanael Mjanael, alipongeza juhudi za wana CCM hao katika kukijenga chama chao.

Alisema: "Kwa hili lililofanyika ni jambo jema na kubwa hasa kwa wana CCM kujitoa na ninapenda kuwakumbushe na wana CCM wengine pia watambue wana wajibu wa kujitolea kukijenga chama chao".

## Wapewa mbinu mbadala kudhibiti ukeketaji watoto

**Na Timothy Itembe,** TARIME

WALIMU wa shule za msingi na sekondari wilayani Tarime mkoani Mara pamoja na watendaji wa kata zinazotekelezwa mradi wa jamii imara wamepewa mbinu mbadala za nidhamu na kudhibiti ukeketaji kwa watoto wa kike.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo yaliyotolewa na shirika lisilo la serikali la Wildaf wilayani Tarime, Ofisa Mradi wa Jamii Imara, Suzan Kawanga alisema mbinu zinazotolewa zinalenga kumsaidia mwalimu kusimamia vema darasa na kuwalinda watoto dhidi ya ukatili.

Kadhalika alisema wanamjengea mwalimu mazingira ya kujifunza mbinu salama na mbadala ya adhabu za kimwili kama vile kazi za kijamii, majadiliano ya pamoja, shughuli za kujenga uhusiano mzuri kati yao na wanafunzi.

Mtoa mada katika mafunzo hayo, Thomas Mponda alisema kwa walimu walezi wanatakiwa kutambua mbinu bora za malezi kwa wanafunzi na jinsi ya kujihami na ukatili wa kijinsia hususani ukeketaji.

Mponda alisema lengo la kuwaweka pamoja walimu, viongozi wa serikali pamoja na kinamama ni kuhakikisha watoto wanakuwa salama dhidi ya ukatili wa ukeketaji kwani hayo ndiyo maeneo yanayomzunguka kila siku.

Mtendaji Kata ya Komaswa, Joyce Mwita aliomba Bunge kutunga sheria kali dhidi ya ukatili kwa watoto na wanawake ili kuwaadhibu wote wanaojihusisha na vitendo hivyo na kuomba elimu iendelee kutolewa kwa jamii.

Baadhi ya washiriki katika mafunzo hayo, Anna Nyamohanga alisema kuwa wazazi wanapaswa kuwasomesha watoto wa kike ili waondokane na tabia ya kuwakeketa.

## DC Mtatiro amjibu Askofu Bagonza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, amejibu kauli iliyotolewa hivi karibuni na Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza kuhusu viongozi wanaosema kila kitu kimefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo wao kukosa haki ya kuendelea kuaminiwa.

Akijibu hoja hiyo, Mtatiro alisema sababu ya viongozi kufanya hivyo kila wanaposimama kwenye majukwaa ni kutokana na Rais Samia ndiye kiongozi wa nchi na majukumu yake yanatambulika kikatiba, kama mpitishaji wa kila bajeti inayopelekwa bungeni na kuzifanyia kazi.

Alitoa kauli hiyo juzi kwenye mkutano wa hadhara, uliofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Town Manispaa ya Shinyanga na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo madiwani na mbunge wa Shinyanga, Patrobas Katambi.

"Kuna watu, tena na juzi nimemsikia kiongozi mmoja tena ana heshimika, anasema watu wanajikomba sana kwa Rais na Mwenyekiti wa CCM, eti kwa sababu kila kiongozi akisimama jukwaani anasema hili limefanywa na Rais, hebu niwakumbushe hii nchi inaongozwa na nani, bajeti zote ambazo zinapelekwa bungeni kupitishwa zinafanyiwa kazi na kuandaliwa na nani, kwa mujibu wa katiba yetu Rais ndiye kila kitu," alisema Mtatiro.


Aidha, alisema kila kitu kinachofanywa, amani pamoja na kodi ambazo hulipwa na wananchi, Rais ndiye anapanga na kwamba haiwezekani kusema mafanikio yaliyopo hapa nchi yanaletwa na kila mtu tu, na ukimtaja Rais wa Tanzania unawataja Watanzania wote.

Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, alisema huduma mbalimbali zimeendelea kuboreshwa jimboni humo ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja, ambayo yalikuwa kero kwa wananchi, huduma za afya, elimu ambako zimejengwa shule mpya tatu za sekondari.

Nipashe
# Spotika



LUIS SUAREZ ... UKURASA 14



VINICIUS

BELLINGHAM



MBAPPE

# NYOTA 5 WENYE NAFASI KUBWA YA KUTWAA BALLON D'OR 2024

**PARIS,** Ufaransa

WAGOMBEA wa tuzo ya Ballon d'Or 2024 wamebainika, huku mshindi akitarajiwa kutangazwa Oktoba 28, mwaka huu, jijini Paris, Ufaransa.

Jumla ya wachezaji 30 waliofanya vema zaidi msimu wa 2023/24, wamepata kibali, huku mjadala mwingi ukiendelea kuhusu nani anastahili kushinda tuzo hiyo.

Ili kupata burudani, hapa 90min imeamua kuwa na nafasi ya kuorodhesha walioteuliwa 5-bora kati ya nani anayefaa kushinda tuzo ya Ballon d'Or ya 2024.

**5. Kylian Mbappe**

Kylian Mbappe anaweza kuwa mwanasoka mwenye kipaji kikubwa zaidi duniani, lakini hakuwa mwanasoka bora zaidi duniani wakati wa msimu wa 2023/24.

Hiyo inasemwa, akiwa amefunga mabao 44 katika michezo 48, alikuwa karibu sana kuwa bora zaidi.

**4. Lamine Yamal**

Lamine Yamal ambaye anapewa nafasi kubwa zaidi ya kushinda taji la Kopa (mchezaji chipukizi), anapaswa kupata kura chache za kutosha za Ballon d'Or mwaka huu pia. Ambayo, ndio, kwa sababu ana umri wa miaka 17.

**Kinda huyo alijiimarisha kama supastaa wa kweli wa soka dunia mnamo 2023/24 licha ya umri wake mdogo, aliisaidia Hispania kutwaa ubingwa wa Euro 2024.**

**3. Jude Bellingham**

Kwa muda mrefu wa msimu uliopita, Jude Bellingham alionekana kuwa na uhakika wa kushinda Ballon d'Or.

Mwishowe, hata hivyo, kudorora kwake kidogo kwenye kampeni kumemfanya aanguke chini kidogo.

Bado, hata hivyo, idadi kubwa ya mabao aliyofurahia mapema msimu wa 2023/24, inapaswa kutosha kumpatia za Ballon d'Or mwishoni mwa Oktoba.

Mabao 23 kutoka kwa safu ya kiungo ya kushambulia hakika si kitu cha kunuswa hata kidogo.

**2. Rodri**

Hakuna mwanasoka duniani anayehakikisha ushindi kama Rodri.

Iwe katika kiwango cha klabu akiwa na Manchester City - ambapo alishinda taji lingine la Ligi Kuu England - au katika kiwango cha kimataifa akiwa na Hispania - ambapo alishinda Euro 2024 - uwapo mkubwa wa Rodri katikati ya uwanja unahakikisha mataji kwa timu yoyote anayochezea.

Ni kiungo wa kati wa ajabu kabisa, na ni mmoja wa wanaopendekezwa kushinda Ballon d'Or mwaka huu.

**1. Vinicius Junior**

Fowadi huyo mpana hakuchezeka kabisa ilipokuwa muhimu zaidi kwa Real Madrid msimu uliopita, alifunga mabao matatu katika nusu fainali na fainali ya Ligi ya Mabingwa na kutwaa taji hilo kwa mara ya 15 ikiwa ni rekodi.

Hakuna mchezaji aliyeongeza kasi katika michezo mikubwa jinsi Vini alivyofanya katika msimu wote wa 2023/24.

## ISIKUPITE

Cristiano Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 900 ya kiwango cha juu katika maisha yake ya uchezaji wakati ikiiwezesha Ureno kuanza vema Ligi ya Mataifa ya Ulaya kwa ushindi dhidi ya Croatia. Mabao 900 ya Ronaldo mwenye umri wa miaka 39, yamekuja kwa aliyofunga akiwa Sporting Lisbon, Manchester United, Real Madrid, Juventus na hivi karibuni Al-Nassr ya Saudi Arabia.



# 10 BORA YA MABEKI WA KULIA WA MUDA WOTE EPL



WALKER

**LONDON,** England

SOKA limebadilika sana katika muongo mmoja uliopita, lakini moja ya mabadiliko makubwa yamekuja katika idara ya beki wa pembeni.

Mabeki wa kulia na wa kushoto hawawezi tena kusimama wakizungusha vidole gumba kwenye mstari wa nusu, wakirudi nyuma kwa hamaki mara tu upande wao unapoacha kumiliki. Badala yake, lazima wawe washambuliaji na wapiga pasi, wakishangilia kwa mabao na kutoa pasi za mabao pamoja na majukumu yao magumu ya ulinzi.

Ushahidi wa mabeki hao wa pembeni wa kisasa umeenea katika Ligi Kuu England, EPL.

Hawa ndio mabeki bora wa kulia wa wakati wote wa Ligi Kuu England, wa zamani na wa kisasa...

**#10. Steve Finnan**

Steve Finnan alikuwa mwingine nje ya mstari wa uzalishaji, akitumia enzi yake na Liverpool katikati ya miaka ya 2000.

Alikuwa mtoa huduma wa kutegemewa kwa Gerard Houllier na Rafael Benitez, akijivunia kiatu cha kulia ambacho kingeweza kupata kichwa cha mshambuliaji yeyote ndani ya eneo la hatari - kwa urahisi zaidi Peter Crouch.

Finnan alisifika kwa kupiga mpira kwenye ubavu wa kulia, ustadi aliouboresha akiwa Fulham kabla ya kuhama Anfield. Mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA.

**#9. Bacary Sagna**

Sawa na mwenzake wa pembeni Gael Clichy, Mfaransa Bacary Sagna aligawanya siku zake kwenye Ligi Kuu England kati ya Arsenal na Man City, akihama kutoka ya zamani hadi ya mwisho mnamo 2014.

Hata hivyo, ilikuwa ni kwa 'Washikabunduki' ambapo Sagna alivutia zaidi, akitoa maonesho mazuri kwenye upande wa kulia wa safu ya ulinzi ya kocha Arsene Wenger.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa alistahili kurudisha muda katika maisha yake ya soka nchini Uingereza akiwa na zaidi ya Kombe la FA na Kombe la Ligi katika kabati lake la mataji.

**#8. Cesar Azpilicueta**

Mabeki wa pembeni ni sawa na kuvaa mioyo yao kwenye mikono yao na Cesar Azpilicueta alitoa mfano huo zaidi ya wengi. Mhispania huyo asiyechoka angefanya lolote ili kupata ushindi, hata kama ingemaanisha kufunika kila majani na kuuweka mwili wake katika hatari.

Hata hivyo, ni rahisi kusahau jinsi mwanasoka mwenye kipawa cha kiufundi Azpilicueta alivyokuwa Chelsea. Alitoa mabao kumi na asisti 36 katika mechi 349 za Ligi Kuu England na alionesha uwezo wa kucheza kama beki wa pembeni au beki wa kati.

Nahodha wa Chelsea kwa miaka mingi, alinyanyua taji la Ligi Kuu mara mbili.

**#7. Lauren**

Lauren alikuwa sehemu ya kikosi cha Arsenal ambacho kilifikia kilele kipya mwanzoni mwa miaka ya 2000, akitamba katika kikosi cha kwanza chini ya Wenger baada ya msimu wa kwanza kutetereka huko Highbury. Kupanda kwa Mcameroon huyo kulikuwa muhimu sana kwa 'Washikabunduki' kutwaa mataji mawili ya Ligi Kuu England, ikiwa ni pamoja na msimu wa Invincibles wa 2003/04.

Alikuwa mtoa huduma hodari katika nafasi ya tatu ya mwisho lakini pia alitoa usaidizi wa mashambulizi.

#6. Branislav Ivanovic

Ukifungua kichwa cha Branislav Ivanovic, ungekuta zege imara. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Serbia alifika mara kwa mara kwenye nguzo ya mbali ili kutoa mguso muhimu ndani ya eneo la hatari.

Ingawa alikuwa mlinzi mzuri pia, ilikuwa ni milipuko yake ya nguvu ndani ya eneo la hatari na mapigo ya kukaba yaliyomfanya apendwe na mashabiki wa Chelsea, akiwa na mabao 22 kwenye Ligi Kuu.

Ivanovic alikuwa na uwezo wa miguu yake pia, mara nyingi akipata mchezaji mwenzake au nyuma ya wavu kwa kuzungusha kiatu chake cha kulia.

**#5. Pablo Zabaleta**

Pablo Zabaleta alikuwa mwanasoka mahiri. Alikuwa mzuri katika kulinda, mzuri kwenye mpira na mzuri kwenda mbele. Nini zaidi unaweza kuomba kutoka kwa beki wako wa kulia, eh?

Akiwa na ucheshi mwingi wa Amerika Kusini na kiwango cha kufanya kazi bila kuchoka, Muargentina huyo aliabudiwa kwa miaka tisa akiwa na Man City na alionekana kuwa muhimu katika kuinuka kwao kwa ubora.

Alifunga hata siku mashuhuri zaidi katika historia ya klabu hiyo, akitoa la kwanza katika ushindi maarufu wa 3-2 dhidi ya Queens Park Rangers ambapo bao la dakika za lala salama la Sergio Aguero liliipa Man City ubingwa wa taji la Ligi Kuu England.

**#4. Lee Dixon**

Lee Dixon hajafanya sifa yake kwa upendeleo wowote kwa kazi yake ya udadisi, lakini bado alikuwa mwanasoka mzuri. Akiiwakilisha Arsenal kwa miaka 14 na kwa misimu kadhaa kabla ya kuanzishwa kwa Ligi Kuu, Mwingereza huyo mara kwa mara alikuwa akicheza safu ya ulinzi.

Alishinda taji la Ligi Kuu England mara mbili huku 'Washikabunduki' wakiwa wamenyanyua mataji mawili ya Ligi Daraja la Kwanza hapo awali, akiwa katika safu ya kushangaza pamoja na Nigel Winterburn, Steve Bould na Tony Adams.

Dixon halikuwa jina la kupendeza na aliweza kutegemewa kufanya kila kitu kinachohitajika kwa beki wa pembeni katika siku za mwanzo za Ligi Kuu.

**#3. Trent Alexander-Arnold**

Kutoka kwa uthabiti wa kuvutia, Trent Alexander-Arnold ameandika tena kitabu cha sheria kwa mabeki wa kulia tangu ajitokeze kwenye eneo la tukio.

Mlinzi huyo wa Liverpool mara nyingi amekuwa akishutumiwa kwa kujilinda lakini bila kujali kama hiyo ni kweli, yeye ni kipaji wa kizazi ambaye alilipuka chini ya Jurgen Klopp.

Beki wa kulia aliye na asisti nyingi zaidi katika historia ya Ligi Kuu England, Alexander-Arnold ana pasi nyingi na ana uwezo wa kuweka mpira kwenye ndani ya sita.

Ujanja na uwezo wake wa kupiga pasi usio na kifani unamfanya kuwa miongoni mwa mabeki wenye vipaji vingi kuwahi kushika nafasi hiyo kwenye Ligi Kuu.

**#2. Gary Neville**

Jamie Carragher alicheka sana: "Hakuna mtu anayekuwa akitaka kuwa Gary Neville." Hilo linamdhuru kwa kiasi kikubwa beki wa kulia wa Ligi Kuu England na mwenye msimamo thabiti, ambaye alikuwa kiungo muhimu wa timu kadhaa za kipekee za Manchester United.

Hukuweza kuwa na maswali kuhusu ubora wa Gary Neville. Mara nyingi ana hatia ya kudharau mafanikio yake, lakini mzaliwa huyo wa Bury alikuwa mlinzi shupavu sana wa mtu mmoja na mkabaji hodari.

Neville pia alikuwa hodari wa kusonga mbele, akitengeneza pasi 35 za mabao katika maisha yake yote ya Ligi Kuu England na kuelekea kunyakua mataji nane ya ligi akiwa na 'Mashetani Wekundu' hao.

**#1. Kyle Walker**

Mchezo wa riadha wa Kyle Walker umemfanya kuwa tofauti na wenzake katika kipindi cha muongo mmoja uliopita. Kasi na nguvu ya beki wa kulia mara nyingi humfanya kuwa kitu kisichohamishika na kufidia upungufu wowote katika mkusanyiko - vizuri, mara nyingi zaidi.

Huwezi kustawi chini ya Pep Guardiola kwa muda wote ambao Walker amekuwa nao bila kuwa mwanasoka hodari na anaweza kuwa hana kipaji cha kiufundi kama mastaa wengine wa Man City, lakini uzoefu wake, uongozi na umbile lake ni zaidi ya kufidia.

Mataji sita ya Ligi Kuu England yanajieleza yenyewe, huku Walker akiwa mmoja wa mabeki bora zaidi ambao tumemshuhudia katika Ligi Kuu England.

## Nukuu

"Suala ni kwamba UEFA na FIFA wanaendelea kuongeza mechi za ziada, na tunaweza kuibua wasiwasi, lakini hakuna suluhu iliyopatikana. Inaonekana kwamba fedha huzungumza zaidi kuliko sauti za wachezaji," **Kevin De Bruyne, akiibua wasiwasi juu ya athari za kalenda iliyojaa kwenye afya na uchezaji wa wachezaji.**



"Bibi na Babu yangu kwa upande wa baba yangu wote ni Wa-Ireland, wameshakufa na hawapo tena kwa hivyo nadhani kusherehekea bao kungekuwa ni kukosa heshima, sikutaka kufanya hivyo. Sina neno baya la kusema na ninawatakia kila la heri kama nifanyavyo mara zote," **Declan Rice, baada ya kufunga bao wakati England ikiibuna na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Ireland na kuamua kutokushagilia.**



"Real Madrid ina wachezaji wakubwa. Lazima uweze kuleta ubora wako katika huduma ya klabu. Hicho ndicho tunachojaribu kufanya kila mwaka. Mwaka huu, wachezaji wapya kama Kylian [Mbappe] na Endrick wanabadilika vizuri sana. Tutakuwa na msimu mzuri wa kushindana katika mashindano yote," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti.**




Kikosi cha Yanga

# TIMU TANO ZENYE NAFASI YA KUCHEZA KIMATAIFA 2025/26

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25 iliyoanza Agosti 16, itaendelea tena keshokutwa, Jumatano kwa michezo mbalimbali ya baadhi ya mechi za raundi ya pili, pamoja na kuanza kwa raundi ya tatu.

Timu 16 zitamenyana kwa msimu mzima kusaka Bingwa wa Tanzania Bara ambaye ataiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Mbali na bingwa, timu itakayomaliza nafasi ya pili itapata nafasi sawa kama ya bingwa, kwa kuiwakilisha Tanzania katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutokana na pointi za nchi zilizopo kwenye Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Katika Ligi Kuu Tanzania Bara, nafasi ya tatu inachulikuwa na timu ambayo moja kwa moja inakwenda kuiwakilisha nchi katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Miaka ya hivi karibuni nafasi ya nne imekuwa ikisakwa sana na timu za Ligi Kuu kwa sababu imekuwa na faida tofauti na huko nyuma.

Ni kwamba timu yoyote inayomaliza nafasi hiyo inaombea timu itakayotwaa ubingwa wa Kombe la FA, iwe moja kati ya zile zilizomaliza nafasi tatu za juu. Kwa sababu ndiyo kitu pekee ambacho kitakachoifanya timu hiyo kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mfano msimu huu, Coastal Union imecheza Kombe la Shirikisho Afrika baada ya kushika nafasi ya nne kutokana na Yanga kutwaa kombe hilo wakati huo huo ndiyo Mabingwa wa Tanzania Bara ambao wanakwenda kucheza Ligi ya Mabingwa.

Kanuni zinasema bingwa wa Kombe la FA ataiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, lakini kama itakuwa ndiyo timu iliyotwaa ubingwa wa Ligi Kuu, basi nafasi hiyo itakwenda kwa timu iliyomaliza nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu.

Kitu pekee ambacho kinaifanya timu inayoshika nafasi ya nne isicheze Kombe la Shirikisho Afrika ni ubingwa wa FA kuchukuliwa na timu itakayoshika kuanzia nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu kushuka chini, au timu za madaraja ya chini.

Kutokana na hali hiyo pamoja na ubingwa, timu 16 zinasaka nafasi nne za juu kwa ajili ya kutaka nafasi ya kucheza kimataifa.

Kwa kuzingatia hilo, katika makala haya tunakuletea timu nane zinazopewa nafasi kubwa zaidi ya kumaliza nafasi nne za juu msimu huu, twende sasa...

**5# KMC**

Ilibaki kidogo icheze Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita, baada ya kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu nyuma ya Coastal Union iliyokwenda kuiwakilisha nchi katika michuano hiyo.

Ikumbukwe kuwa KMC ina vinasaba vya kucheza michuano ya kimataifa kwani ilishawahi kufanya hivyo mwaka 2019, ilipocheza Kombe la Shirikisho, ikakipiga dhidi ya AS Kigali ya Rwanda, Agosti 10 ugenini na kulazimisha suluhu, kabla ya kutolewa ikiwa nyumbani Agosti 23, mwaka huo.

Kocha Mkuu, Abdihamid Moalin, amefanya usajili mkubwa msimu huu, kwa wachezaji mbalimbali kutoka Burundi, Rwanda, na Uganda, hivyo ni moja kati ya timu zinazotarajiwa kumaliza ndani ya nne bora msimu huu.

**5# Singida Black Stars**

Ni moja kati ya timu iliyosheheni wachezaji wengi wa kigeni kwenye ubora mkubwa na maarufu ukiziondoka klabu za Simba na Yanga.

Inaonekana kama haitaki utani msimu huu kwani imeshinda mechi zake mbili ilizocheza mpaka sasa, tena ikiwa ugenini.

Iliichapa KenGold mabao 3-1 na kushinda bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, na inazidiwa mabao ya kufunga na Simba tu ikiwa kwenye nafasi ya pili.

**3# Azam FC**

Licha ya kwamba haijawahi kutinga hatua ya makundi katika michezo ya kimataifa, lakini Azam FC, ni moja kati ya timu ambazo hazijawahi kukosa kucheza michuano hiyo, tangu Tanzania ilipoanza kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa.

Pamoja na kutofanya vema, lakini haiondoi kuwa ni timu yenye msuli mkubwa linapokuja suala la miundombinu ya klabu, usajili pamoja na malengo yao, ambayo ni tofauti na baadhi ya timu za Ligi Kuu ambazo zinahubiri kucheza nne bora, lakini ukweli ni kwamba zinachotaka ni kusalia tu kwenye ligi na si vinginevyo, hivyo inatarajiwa pia msimu ujao kuwa moja ya timu zitakazomaliza ndani ya nne bora na kucheza kimataifa.

**2# Simba**

Itakuwa ni maajabu makubwa kwenye soka la Tanzania kama Simba isipomaliza ndani ya nne bora. Msimu uliopita ilipomaliza nafasi ya tatu na kutafsiriwa kwamba ni kufeli kwa kiwango cha juu kwa viongozi, wanachama na mashabiki wake.

Ndiyo maana ilifumua asilimia kubwa ya kikosi chake na kutengeneza kingine kipya. Nia si kumaliza ndani ya nne, bali ni kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara.

Simba ni timu ambayo ligi ikianza si kwamba inataka kumaliza ndani ya nne bora, bali kutwaa ubingwa, nafasi zilizobaki chini yake zote kwake ni kufeli.

**1# Yanga**

Haina mjadala kuwa Yanga itacheza mechi za kimataifa msimu ujao, hata kama isipotwaa ubingwa. Kwa sababu itakuwa ndani ya nne bora. Yanga na Simba ni timu ambazo zinaamini kuwa ubingwa umeumbwa kwa ajili yao.

Kwa sababu ni timu moja itakayoupata, basi nyingine huwa haipo mbali sana na hapo. Kama si ya pili, basi itakuwa ya tatu.

Haishangazi kuona kuwa ndiyo timu iliyotwaa ubingwa mara nyingi zaidi kuliko timu zingine, na huwa zinapokezana tu na Simba.

Yanga iliyotwaa ubingwa mara 30, na bingwa mtetezi, ndiyo timu iliyoiwakilisha Tanzania mara nyingi zaidi mechi za kimataifa, ingawa mafanikio yake huko si makubwa sana kama ilivyo kwa Simba.

**JE, WAJUA?**



Luis Suarez ijumaa iliyopita alihitimisha miaka yake 17 ya kuichezea Uruguay kwa sare tasa dhidi ya Paraguay kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia, ukanda wa Amerika Kusini. Jumatatu ya juma lililopita Suarez (37), alitangaza baada ya mechi hiyo atastaafu soka la kimataifa na ametundika daluga akiwa mfungaji bora wa wakati wote wa Uruguay kwa mabao yake 69 yaliyotokana na mechi 143 alizoichezea tangu Februari 2007. "Uruguay ni kubwa kuliko mchezaji yeyote. Kuanzia kesho (Jumamosi), nitakuwa shabiki mwingine," aliuambia umati.



# UWT yakemea tabia wenyeviti mitaa kuwa mahakimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUKITHIRI kwa matukio ya ukatili wa kijinsia, ubakaji na ulawiti, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Mary Chatanda amekemea tabia ya wenyeviti mitaa kujigeuza mahakimu, akisema hiyo sio kazi yao bali waviachie vyombo vya sheria.

Aidha, ameitaka Kamati ya Haki na Sheria ya UWT, wadau na wabunge kufanya tathmini ya kina ili kujua sababu za kuongezeka vitendo hivyo licha ya kuwapo na adhabu kali.

Alisema hayo jijini hapa baada ya kuzindua kamati hiyo sambamba na kampeni ya msaada wa kisheria chini ya UWT.

Chatanda alisema mwenyekiti yeyote wa kijiji atakayebainika kushiriki kuzima kesi za vitendo hivyo watahakikisha anachukuliwa hatua.

Aidha, alisema tathmini hiyo ilenge kuona vifungu vya sheria vinavyohusika na makosa ya ubakaji na ulawiti kama vinahitaji marekebisho ya sheria na kutoa mapendekezo kwa serikali.

**"Inasikitishwa na matukio haya ikiwemo ya hivi karibuni ya mtoto wa miezi sita kulawitiwa na kubakwa na baba yake mzazi hapa Dodoma hali iliyopelekea kifo cha mtoto huyo...**

"Inasikitishwa na matukio haya ikiwemo ya hivi karibuni ya mtoto wa miezi sita kulawitiwa na kubakwa na baba yake mzazi hapa Dodoma hali iliyopelekea kifo cha mtoto huyo na tukio la kubakwa na kuawa kwa mama na binti yake, UWT inalaani matukio haya na kuiomba serikali yetu kuendelea kutafuta mwarobaini wa matukio haya ya kusikitisha," alisema.

Alisema UWT imekuwa mstari wa mbele katika ajenda ya kuhimiza maadili katika jamii na kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake ambapo ni moja ya kipaumbele chake.

Hivyo, alihimiza utoaji elimu kwa Watanzania nchini juu ya ukatili wa kijinsia na wanawake wasifumbie macho vitendo hivyo hata kama vinafanywa na wanaume zao.

Hata hivyo, alisema kufanyika kwa kampeni hiyo ni kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutoa huduma ya msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia.

Mwenyekiti wa kamati hiyo na Naibu Waziri TAMISEMI, Zainab Katimba alisema imeanzishwa kampeni ya msaada wa kisheria itakayoanza kwenye mikoa 10 na kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kwenye ofisi za UWT kutakuwa na watoa msaada kisheria.

Alisema wanawake, watoto na watu wenye mahitaji maalum ndiyo walengwa kwenye kampeni hiyo na wameandaa programu maalum kufikia watoto shuleni ili kupata elimu ya kujilinda na ukatili.

## Vijiji 34 Mufindi, Kilolo vyaondokana na kero ya maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Rural Development Organisation (RDO) limevifikia vijiji 34 vya Wilaya ya Mufindi na Kilolo mkoani Iringa, kuviondolea adha ya upatikanaji wa maji kwa wanawake wa maeneo hayo.

Mkurugenzi wa RDO, Fidelisi Filipatali aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu programu ya maji wanayoifanya katika maeneo mbalimbali.

Alisema wameamua kufanya utekelezaji wa mradi huo wa maji katika maeneo hayo ili kuisaidia serikali kwenye uwekezaji wa maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Alisema limesambaza mabomba ya maji kwenye vijiji, hivyo ili kuhakikisha suala la maji linatatuliwa na kuwatua ndoo kina mama kichwani.

Dendego alisema shirika hilo limekiwa likitoa mafunzo ya ufundi kwa vijana ili kujiajiri wenyewe katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Alieleza kuwa Mkoa wa Iringa pia wanatekeleza miradi mbalimbali ya kuwainua kiuchumi Watanzania.

Hata hivyo alisema wanajipanga kuona namna ya kutanua wigo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na serikali ili kuhakikisha vijana wanainuka kiuchumi kwa ujasiriamali wanaofanya.

Msajili msaidizi wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika Halmashauri ya Mufindi, Suzana Kapungu alisema RDO imesaidia suala zima la upatikanaji wa maji katika wilaya hizo.

Kapungu alisema wamekuwa wakishirikiana vizuri na shirika hilo, huku akisisitiza ushirikiano wataendelea nao hadi kwenye utoaji mafunzo kwa vijana wanaochipukia katika fani mbalim





Wakili wa Serikali Wizara ya Katiba na Sheria,Innocent Magesa (kushoto) akimpa msaada wa kisheria, Fauzia Ally wakati wa uzinduzi wa huduma ya msaada wa kisheria iliyoandaliwa na Kamati ya Haki na Sheria ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Chama Cha Mapinduzi (CCM). Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mifuko ya programu uwezeshaji wananchi kukutana

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MIFUKO na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zaidi ya 20 inatarajia kushiriki maonesho ya saba ya kitaifa ya mifuko hiyo yanayofanyika kuanzia Septemba 8 hadi 14 mwaka huu mjini Singida.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego akizungumza jana alisema maonesho hayo yatafunguliwa kesho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi na yatafungwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema Mkoa wa Singida umejiandaa kikamilifu kuwa mwenyeji wa maonesho ambapo maandalizi yote muhimu yamekamilika ili kuhakikisha wageni kutoka mikoa mbalimbali wanapokelewa na kuhudumiwa vizuri.

Dendego alisema lengo la maonesho hayo ni kuwaletea wananchi wa Mkoa wa Singida na mikoa jirani na Watanzania kwa ujumla taarifa sahihi za mifuko hiyo ya uwezeshaji na programu zake ili waweze kunufaika nazo.

Alisema wafanyabiashara wa Mkoa wa Singida watumie fursa ya maonyesho hayo kuuza bidhaa zao na kutoa huduma nzuri na kuepuka upandishaji wa bei usioeleweka ili wageni watamani kurudi tena Singida.

Alisema maonesho haya yanatoa nafasi ya pekee kwa wananchi kupata uelewa wa kina kuhusu programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi na jinsi wanavyoweza kunufaika nazo

Dendego alisema, serikali ya mkoa imejipanga kikamilifu ili kuhakikisha usalama wa wageni na washiriki wote wa maonesho hayo, lengo likiwa ni kuboresha nafasi ya Singida kama kituo cha mikutano na maonesho.

Naye, Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, alisema kuwa maonesho hayo yatakuwa na taasisi nyingi zinazotoa mikopo na ruzuku kwa ajili ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

## Wadau, serikali wajadili utekelezaji wa mikataba

**Na Mwandishi Wetu,** Dodoma

WADAU wa maendeleo kupitia mradi wa USAID Afya Yangu Kanda ya Kusini, wamekutana na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuangalia namna bora ya kurahisisha utekelezaji wa mikataba.

Mradi wa USAID Afya Yangu unafadhaliwa na PEPFAR kwa kupitia USAID na kusimamiwa na Deloitte Consulting Limited na washirika wenza MDH na TMARC Tanzania

Akizungumza wakati wa kikao hicho Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Rashid Mfaume alisema kuwa wadau pamoja na serikali waliona ni vyema kukutana na kujadili namna bora ya kurahisisha utekelezaji wa mikataba.

Alisema katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 mradi unatarajia kufanya uwekezaji katika huduma za VVU/UKIMWI, TB, na uzazi wa mpango kwa kuingia mikataba na mikoa sita, halmashauri 43, hospitali za rufaa sita.

Kikao hicho kiliwashilikisha maofisa kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, waganga wakuu wa mikoa, wilaya na halmashauri, wamanasheria wa mikoa, wilaya na halmashauri pamoja na maofisa wa mradi wa USAID Afya Yangu Kanda ya Kusini,

Mradi huo ni wa miaka mitano, kwamba unalenga kusaidia serikali kutoa huduma bora jumuishi ya matunzo, matibabu, na kuzuia VVU na kifua kikuu ambazo zitaboresha matokeo ya afya, hasa kwa vijana na watoto katika mikoa sita ya Iringa, Lindi, Morogoro, Mtwara, Njombe and Ruvuma.

Mkurugenzi Mkuu wa Mradi wa USAID Afya Yangu, Dk. Marina Njelekela alisema mradi huo unatoa msaada wa kiufundi na nyenzo na msaada wa kiutawala na usimamizi kwa Tanzania kupitia TAMISEMI.

Alisema lengo ni kuongeza uwezo wao wa kusimamia na kutoa huduma bora za VVU na kifua kikuu ndani ya sekta ya umma na vituo vya afya vinavyohusiana na imani.

Alisema mradi huo unaimarisha utoaji wa huduma za afya katika jamii kwa kuunganisha na kuboresha uhusiano kati ya jamii na vituo vya afya.

Alisema: "Malengo ya mradi ya USAID Afya Yangu Kanda ya Kusini ni kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya zinazomlenga mtumiaji, kuboresha uwezo wa mtu mmoja mmoja kufuata tabia njema za kiafya pamoja na kuboresha mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora za afya".





Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege, akikagua kiwanda cha kusaga unga wa sembe cha Chama Kikuu cha Ushirika wa wakulima wa Tumbaku wilayani Chunya (CHUTCU) kilichopo katika Kata ya Lupatingatinga alipofanya ziara mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TCDC yataja mbinu kudhibiti wizi katika tumbaku

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

VYAMA vya msingi vya wakulima wa tumbaku nchini vimetakiwa kuwasajili wanachama wao kwa mfumo wa kielektroniki, ili kudhibiti udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wanachama na kuvisababishia hasara.

Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa anakabidhi magari mawili ambayo yamenunuliwa Chama Kikuu cha Ushirika wa wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya (CHUTCU).

Alisema vyama vingi vya msingi wanachama wake hawajasajiliwa na hawatambuliki kwenye mfumo wa kielektroniki, hali ambayo inasababisha kuwepo kwa udanganyifu wakati wa kuuza mazao yao na kusababisha madeni.

Hivyo, alivitaka vyama hivyo kushirikiana na warajisi wasaidizi wa vyama vya ushirika kuwasajili wakulima na kuwapatia kadi ambazo zitatumika kuwatambua na kudhibiti utoroshaji wa mazao.

Alisema udanganyifu unaofanywa na wakulima unavisababishia vyama hivyo kuwa na madeni kwenye taasisi mbalimbali za kifedha zikiwemo benki ambazo huwa zinakopesha pembejeo za ilimo na ujenzi wa miundombinu.

Aliwashauri viongozi wa AMCOS kuwatumia vijana waliohitimu vyuo vikuu na hawana ajira kuwasajili wakulima kwenye mfumo huo ambao alidai ndiyo suluhu ya kudumu ya udanganyifu.

> **Mwenyekiti wa Bodi ya CHUTCU, Sebastian Masika alisema ununuzi wa magari hayo utamaliza uhaba wa vyombo vya usafiri uliokuwepo kabla ya magari haya kununuliwa.**

Meneja Uendeshaji wa CHUTCU, Juma Nshinshi alisema ununuzi wa magari hayo mawili yameghalimu zaidi ya Sh. milioni.400 ambazo zinatokana na mapato ya ndani ya chama hicho.

Alisema bodi ilipeleka wazo la ununuzi wa magari hayo kwa wanachama kwenye mkutano mkuu na wanachama walilidhia taratibu za manunuzi ziendelee ili kurahisha usafiri wa kuwafikia wakulima kwenye maeneo yao.

Alisema mpaka sasa AMCOS ambazo ni wanachama wa CHUTCU ziko zaidi ya 18 na nyingi ziko maeneo ya vijijini hali ambayo inahitaji kuwa na magari yenye yenye ubora ili kuzifikia.

Mwenyekiti wa Bodi ya CHUTCU, Sebastian Masika alisema ununuzi wa magari hayo utamaliza uhaba wa vyombo vya usafiri uliokuwepo kabla ya magari haya kununuliwa.

Aliwashukuru wanachama kwa kupitisha pendekezo la ununuzi wa magari hayo kwa maelezo kuwa uwepo wa magari hayo utawasaidia pia wakulima hao kupunguza matatizo yanayowakabili.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Chunya, Anakleth Michombero aliwapongeza viongozi wa CHUTCU kwa kusimamia vyema mali za chama hicho akidai

## Coca Cola kuwakusanya wapishi bora wa vyakula, muziki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Coca-Cola imezindua tamasha la chakula lijulikanalo kama 'Coca-Cola Food Fest' kwa lengo la kuwaleta pamoja wapishi bora wa vyakula, muziki na burudani.

Meneja Chapa na Masoko Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo, alisema tamasha hilo lilizinduliwa mwishoni mwa wiki, linatarajia kuanza leo hadi Novemba 23, mwaka huu.

Alisema tamasha hilo ni kumbukumbu ya urithi wa vyakula mbalimbali na litahusisha wachuuzi wa vyakula vya ndani, watu mashuhuri, wapishi, na maonyesho shirikishi ya kupikia na madarasa bora.

Nshimo alisema wahudhuriaji watapata fursa ya kupima vyakula vitamu kutokana kwa vyakula mbalimbali, vyote vikiwa vimeunganishwa kikamilifu na vinywaji wapendavyo vya Coca-Cola.

Alisema: "Tunafuraha kubwa kutambulisha tamasha la Coca-Cola Food Fest, tukio la kipekee linaloakisi dhamira yetu ya kuwaleta watu pamoja kupitia uzoefu wa pamoja na vyakula vyenye ladha nzuri"

Alisema tamasha hilo litatoa jukwaa la kuonyesha ushirikiano wa kipekee na kuendeleza michanganyiko mipya ya kusisimua inayowafurahisha wateja.

Alisema wapishi mashuhuri watashiriki utaalamu wao kupitia maonyesho ya moja kwa moja ya upishi na madarasa bora, wakionyesha mapishi ya kibunifu ambayo yanajumuisha bidhaa za Coca-Cola.

# Homera: Wafanyabiashara watumieni wataalamu kutoka CBE

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera amewahamasisha wafanyabiashara na wawekezaji wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuwatumia wataalamu kutoka Chuo cha Maendeleo ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mbeya kuboresha shughuli zao.

Pia amewataka kuwatumia wataalamu wa manunuzi, ugavi na uhasibu wanaohitimu katika chuo hicho.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika chuo hicho kwa lengo la kukagua shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu mipya.

Pia, aliwataka wawekezaji hao kuwatumia wataalamu wanaohitimu masomo yao chuoni hapo hasa wa ugavi na manunuzi pamoja na wahasibu.

"Nipongeze sana uongozi wa CBE kwa kuanza udahili wa masomo hayo kwa mwaka 2024, hii itakuwa chachu kubwa kwa taifa na kuwezesha kuchochea uchumi endelevu na ajira kwa vijana watakaohitimu," alisema Homera Homera alisema tangu kuanza kwa chuo hicho miaka 10 iliyopita huu ni mwaka wa kwanza kuanza udahili wa masomo hayo na kuwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo kwa kuunga mkono jitihada za serikali.

Mkurugenzi wa chuo hicho, Jeremiah Wilhelm alisema uwekezaji unaofanywa na serikali kwenye chuo hicho ni kivutio kwa wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuchangamkia fursa za elimu ya biashara.

Alisema ili kufikia malengo ya vijana kujiajiri chuo hicho kimewafikia wajasiriamali 600 kwa mwaka wa fedha 2022/23, kuwapatia elimu ya biashara bure kwenye mitaa, kwenye masoko na kwenye maeneo ya mikusanyiko ya vijana hasa vijiweni.

Alisema sasa hivi wameshapata mzabuni ambaye atakuwa anawauzia chakula watumishi na wanafunzi wa chuo hicho na hivyo uongeza ubora wa elimu.

# RC avihakikishia vyama vya siasa uchaguzi wa huru, haki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imevihakikishia vyama vya siasa mkoani humo kuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakuwa huru na wa haki.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki ofisini kwake wakati wa hafla ya kumuapisha Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas.

Pia alivitaka vyama vya siasa kuchagua viongozi wenye sifa ili wananchi wapate watu sahihi watakao simamia vizuri fedha za miradi na kuchochea maendeleo.

Mtaka alisema kiu yake ni kuona kwamba viongozi watakaopewa dhamana kwenye vijiji na mitaa wanakuwa na mchango mkubwa kwa serikali na wananchi katika kutatua kero.

Mtaka alitoa rai kwa wakuu wa wilaya kwenda kusimamia vizuri miradi ya mendeleo ambayo imeletwa na serikali ili kuweza kutoa matokea mazuri kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Olivanus Thomas alisema anakwenda kutekeleza mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan anapenda kuyaona katika wilaya hiyo yanafanikiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda alisema Mkoa wa Njombe unajipambanua katika mambo mengi ikiwemo ajenda ya udumavu ambayo mkuu wa mkoa ndiye balozi.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zakaria Mwansasu alisema amejipanga kuhakikisha anakwenda kuitekeleza vema ilani ya CCM na kuwaletea maendeleo wananchi.





# Soko la dunia lapandisha bei ya petroli Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya mafuta ya petroli visiwani Zanzibar imepanda katika kipindi cha Septemba kutoka Sh. 3,062 iliyokuwa Agosti hadi Sh. 3,164, likiwa ni ongezeko la Sh. 102.

Akitangaza mabadiliko ya bei hiyo, Meneja Uhusiano kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mbarak Hassan Haji alisema bei ya petroli imepanda kutokana na wastani wa mabadiliko ya bei za mafuta duaniani.

Meneja huyo alisema kuwa bei ya mafuta ya dizel imepungua kwa kipindi cha Septemba ambapo itauzwa kwa shilingi 3,247 kwa lita moja kutoka bei ya awali ya Sh. 3,259 sawa na upungufu wa shilingi 12.


Aidha alisema kwa bei ya mafuta ya taa kwa mwezi huu yatauzwa shilingi 3,200 sawa na bei ya Agosti ambapo bei ya mafuta ya ndege kwa Septemba ni 2,837 na Agost ilikuwa 2,843 tofauti ikiwa ni shilingi sita.

Meneja huyo alitaja sababu zingine za kupanda na kupungua kwa nishati hiyo ya mafuta ni gharama za uingizaji mafuta katika Bandari ya Dar es salaam na Tanga, gharama za mabadiliko ya fedha za kigeni zinazonunulia mafuta, gharama za usafiri, bima, kodi na tozo na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Hata hivyo alisema sababu ya kupungua kwa bei ya dizeli na mafuta ya ndege kwa mwezi huu wa Septemba ni kupungua kwa bei katika soko la dunia.

Alisema sababu ya kuongezeka kwa bei za mafuta ya petroli ni kuongezeka kwa gharama katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za uagizaji hadi kufikia Zanzibar pamoja na mabadiliko ya fedha za kigeni kwa shilingi ya Tanzania.

Alisema: "Mamlaka inawahimiza wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti za kieletroniki kila wanaponunua mafuta".



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk Doto Biteko akikabidhi mtungi wa gesi ya Oryx kwa mmoja wa baba lishe jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dk Ashatu Kijaji (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya OryxGas Tanzania Benoite Araman. Jumla ya mama na baba lishe 2000 wamepatiwa mitungi ya gesi ambapo Oryx wametoa mitungi 1000 na Total mitungi 1000 baada ya kuoneshwa video ya Rais Samia Suluhu Hassan akipika kwa kutumia nishati safi kupitia kipindi cha Azimio la Kizimkazi. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali yawatoa hofu wananchi usalama baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais , Tawala za Mikoa , Serikali za Mitaa Idara Malum za SMZ, Issa Mahfoudhi Haji amesema mipaka ya bahari nchini iko salama.

Alisema hayo wakati akifunga mafunzo kwa askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji eneo la Kikweni Wilaya ya Magharibi A Unguja.

Alisema kuwa askari wa ukoaji na wanamaji wanafanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kuwa mipaka ya bahari inakuwa salama wakati wote, hivyo kuna kila sababu ya kupongezwa kwa kazi yao nzuri .

Alisema kuwa uamuzi wa taasisi ya zimamoto na uokozi ya Tanzania kuwaleta askari wake kupatiwa mafunzo ndani ya Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) ni uamuzi sahihi na inaonesha ushirikiaano uliyopo baina ya taasisi mbili hizo.

Alisema kuwa KMKM kinauweledi mkubwa katika kuwapatia mafunzo ya uogeleaji kwa wanajeshi wake na hata wanaotoka Tanzania Bara na hiyo siyo mara ya kwanza kwa kikosi hicho kutoa mafunzo kama hayo.

Alisema kuwa katika kufikia malengo ya kuendelea kuwa na kikosi bora wizara hivyo itatoa ushirikiano wa kutafuta vifaa vya kisasa, ili kuendelea kutoa mafunzo bora kwa wanafunzi wanokwenda kujifunza fani ya uokozi .

**Alisema kuwa ili kulinda maadili ya watoto lazima wajengewe maadili ikiwamo kumcha Mungu kwa kuwapelekea kusoma elimu ya madrasa.**

Alisema kikosi hicho kinawajibu wa kukaa na taasisi mbalimbali za ulinzi Tanzania ili kubadilishana mawazo juu ya utendaji wa kazi zao.

Mkuu wa KMKM, Azani Hassan Msingiri alisema siyo mara ya kwanza kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuja kujifunza masuala ya uokoaji ndani ya kikosi hicho visiwani Zanzibar.

Alisema kuwa askari hao wamepatiwa mafunzo yote ya uokozi na sasa hivi wako vizuri katika kufanya kazi zao, kwamba wanatakiwa kuaminiwa na kupatiwa vifaa vya kisasa.

Alisema kuwa askari 25 wamehitimu vizuri mafunzo hayo, hivyo wanatoa wito kwa vikosi wengine kuwapeleka askari wao ili kujengwa kisasa katika masuala ya uokoaji na kufanya kazi zao kisasa zaidi.

Naibu Kamishina wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania, Kanedy Komba alisema wataendelea kushirikiana na kikosi hicho ili kuwajenga vizuri askari hao katika fani ya uokozi.

Alisema hiyo ni mara ya pili kwa jeshi hilo kupeleka askari wake kupatiwa mafunzo ya kuogolea na kuokoa ndani kikosi cha KMKM.

Akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi waliohitimu mafunzi hayo, Fadhili Msafiri alisema kuwa katika safari yao ya kujifunza mafanikio makubwa wameyapata ikiwemo kujiamini.

# Wadau: ACT-Wazalendo hakifuati usawa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU wa kutetea haki za wanawake wamesema wanashangazwa na kutofuatwa kwa usawa wa kijinsia katika uongozi kwenye Chama cha ACT-Wazalendo.

Wamesema katika nafasi 16 za uwaziri katika Baraza Kivuli la Mawaziri la chama hicho mwanamke ni mmoja kati ya wanaume 15 walioteuliwa.

Wakizungumza na Nipashe wadau hao walisema kuwa ni vyema vyama vya siasa vikaangalia usawa wa jinsia kwa sababu dunia ndivyo inavyotaka.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar), Dk. Mzuri Issa alisema kuwa kitendo hicho kimewakwaza wanawake kutokana na jitihada zinazofanywa katika masuala ya kijinsia

Alisema ni vyema chama hicho likafumua baraza hilo kwa nafasi za uwaziri na kuwapa nafasi zaidi wanawake, pia kuwajengea uwezo na kuwapa nafasi

"Mwanamke unapompa nafasi anaweza na wanawake wanasifa nzuri kwa sababu hawapendi kujiingiza katika matatizo, hivyo wanahitaji nafasi katika vyombo vya maamuzi" alisema Dk. Mzuri.

Aidha alisema ni vyema wanawake wakaandaliwa kuwa viongozi badala ya kuwaandaa kuwa wapiga kura pekee.

Akitangaza baraza hilo, Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman alisema chama hicho kina sera ya jinsia na wanawathamini na kuwajali wanawake na kuwashirikisha katika mambo mbalimbali ikiwemo ya uongozi.

Alisema wanachokiangalia pia ni uwezo wa wanawake na ndiyo maana wakatoa nafasi nyingi za manaibu waziri katika baraza hilo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**NURU NASHON MWAIKELA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3535/0039/2017** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **DEBRABANT SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017 kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/189926/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHEL ANTON LUVINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1327-0070** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MAZOEZI KLERRUU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/189176**

## KUPOTEA KWA CHETI



**YORKE L. MWAMAPANDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S 1349/0665** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYAKAHURA SECONDARY SCHOO**L mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/190343/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**DEBORA JOSEPH IGAYI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1523-0008** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **AGAPE – MBAGALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014 na **CHETI CHA CHUO CHA GRADE A TEACHER'S CERTIFICATE** chenye usajili namba E0514-0016 kilichotolewa na **ILONGA TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/TEM/92864/2024**

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ORDINANCE**
**(CAP 117)**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 05th day of SEPTEMBER 2024 by me **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI** formerly known as **LEKEI ELIKUNDA MATUU** of P.O. Box Arusha Tanzania, now or until recently called **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI.**


**WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows:

1. I absolutely renounce and abandon the use of my said former name of me **LEKEI ELIKUNDA MATUU,** and I assume and determine to take and use the new name **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI,** in substitution of my former name of **LEKEI ELIKUNDA MATUU** as used in my **PSSF AND IN PURSUANCE** of such change of names(s) as foresaid **I DECLARE** that I shall ta all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the new name of me **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI,** in substitution for my former name of me **LEKEI ELIKUNDA MATUU,** so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid former name, but by the new name of me **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI** only.
2. **AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons of times to describe and address me by the new name of **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI.**

**IN WITNESS** whereof I have hereunto subscribed my new name of me **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI** and have affixed my signature the day and year herein written.

**SIGNED** and **DELIVERED** by the said **ELIKUNDA KAANAELI LEKEI** who is introduced to me by.............................. the later known to me personally in my presence, this 05 day of September 2024.

..................
**DEPONENT**



**BEFORE ME:**
..................
**COMMISSIONER FOR OATHS**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MMASSY AMEDEUS FRANCIS** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 433 CNH – TVS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/191779/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(JUDICIARY)**

**DISTRICT COURT OF KIBAHA**
**AT KIBAHA**

**MSC. CIVIL APPLICATION NO. 15513 OF 2024**

**BANK OF AFRICA..................APPELLANT**

**VERSUS**

**PRISCA MGHAGA.....................RESPONDENT**

**TO: PRISCHA MGHAGA**

You are hereby required (personally) or your representative to appear before this court on 18 day of SEPTEMBER, 2024 at 08:30am before Hon F. KIBONA on such other date or dates to which the suit may stand adjoined, and not to depart without leave of the court.

**AND TAKE FURTHER NOTICE** that if default to appear before this court within the time specified the court may pronounce judgment against you.

GIVEN under my Hand and the Seal of the court, this 6 day of SEPTEMBER, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE OF KIBAHA AT KIBAHA
..............................
**SENIOR RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT MUSOMA SUB-REGISTRY**

**LAND APPEAL NO. 000005848/2024**

**CASE REFERENCE NO. 20240319100005848**

**(Originated from the Decision in the Matrimonial Appeal No. 1 of 2023 In the District Court of Bunda at Bunda, originated from Matrimonial Cause No. 67 of 2023 in the Primary Court of Musoma Urban in the District of Musoma)**

**NALISIS ARCHARD NGEMELA................................ APPELLANT**

**VERSUS**

**MARY HOSEA MAJESHI..............................RESPPONDENT**

**TO: MARY HOSEA MAJESHI**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**WHEREAS** the Applicants have filed the application under certificate of urgency against you, you hereby summoned to appear in this Court in person or by pleader duly instructed and able to answer all material questions relating to the application or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 17th October, 2024 at 08:00 HRS at Tarime before Hon. K. I. Kafanabo, Judge to answer the case.

TAKE NOTICE THAT In default of your appearance on the day before mentioned, the Appeal will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 28th day of August, 2024.

DEPUTY REGISTRAR
Deputy Registrar
High Court of Tanzania
P. O. Box 333, Musoma-Mara

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 111 LA 2024**

**NATURAL CONSTRUCTION COMPANY LIMITED..............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**LEVINA NYINGE T/A MAESA BEATY SHOP..................MDAWIA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**LEVINA NYINGE T/A MAESA BEATY SHOP**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**NATURAL CONSTRUCTION COMPANY LIMITED** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 22/10/2024 saa TATU asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaariwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 26 Mwezi 07, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 141 LA 2024**

**IRENE JAMES RUTA.................MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**GRANITE PROPERTY LIMITED**
**YUSUPH MWINULA GEORGE..................WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

1. **GRANITE PROPERTY LIMITED**
2. **YUSUPH MWINULA GEORGE.........POPOTE MLIPO**

IREINE JAMES RUTA amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 18/09/2024 saa 03:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 18 Mwezi 08, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Nishati chafu ya kupikia yaua watu 33,000 nchini kila mwaka

**Na Gwamaka Alipipi**

WATANZANIA 33,000 wanafariki dunia kila mwaka kutokana na kuvuta moshi na chembechembe zitokanazo na mkaa na kuni.

Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania Ltd, Benoit Araman, alieleza hayo jana wakati wa kampeni ya ‚Pika Kijanja' iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati, akisema kuwa endapo hatua za haraka zisipochukuliwa, hali inaweza kuwa mbaya zaidi miaka ijayo.

Alisema ni wakati mwafaka sasa Watanzania wakaanza kutumia gesi wakati wa kupika.

Araman alisema: „Leo (jana) ningependa kuwasisitiza mamalishe na babalishe walioalikwa hapa leo, ninapenda kuwashukuru kwa kazi mnazofanya kila siku. Mnahakikisha kuwa watu wanakula asubuhi, mchana na jioni. Watu wanaotoka na kwenda kazini, njiani kuelekea shuleni, wakati wa kupumzika, sote tuna fursa ya kuja kwenu na kula chakula kitamu mnachotayarisha."

Alisema matumizi ya nishati safi na kupikia na Oryx LPG hutoa manufaa mbalimbali kwa jamii, wanawake, ukiwamo uboreshaji afya.

Alitaja faida nyingine ni ulinzi wa mazingira, akisema kupika kwa kutumia gesi huzuia ukataji miti, kusababisha kulinda mazingira.

Alitaja faida nyingine ni uboreshaji hali ya maisha, kwamba kupika kwa kutumia gesi kunazuia wanawake kufanya kazi ngumu ya kutumia saa nyingi kukusanya kuni kutoka msituni.

Araman alisema: "Pia kunasaidia kuleta usalama na ulinzi wa wanawake kwa sababu kupika kwa kutumia gesi kutazuia wanawake kukabiliwa na hatari katika misitu ya wanyamapori pamoja na kukutana na watu wabaya wa kuwadhuru."

Faida nyingine ni uwezeshaji wanawake, kwamba kupika kwa kutumia gesi ni haraka na kwa ufanisi, hivyo kutawawezesha wanawake kuwa na muda zaidi wao wenyewe.

Alisema pia kunasaidia elimu ya watoto, akisema kupika kwa kutumia gesi hiyo hakuhitaji watoto kwenda msituni.

Faida nyingine alitaja ni kusaidia kupambana na unyanyasaji kijinsia, akisema wanawake watakuwa na chakula kilichoandaliwa kwa wakati na wanaume hawatalalamika juu ya kuchelewa kwa chakula kinachosababisha mabishano.

Alisema kampuni ya Oryx Gas Tanzania Limited inafanya kazi bila kikomo kila siku ili kutekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwamba asilimia 80 ya Watanzania wapate nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Araman alisema mpango huo utafanikiwa tu ikiwa jamii itajitolea kutumia nishati safi kupikia kila siku.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda (kushoto) akifurahia jambo na Dk Marco Wopereis, Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya World Vegetable Centre (kulia) pamoja na Dk Gabriel Rugalema (kati kati) ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa World Vegetable Centre kanda ya Afrika wakati wa mkutano uliohusu masuala ya chakula barani Afrika uliofanyika Kigali nchini Rwanda mwishoni mwa wiki. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Tume: Hakukuwa na ukiukwaji haki za binadamu upanuzi wa mgodi

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesema hapakuwa na ukiukwaji haki za binadamu wakati wa upanuzi wa eneo la uchimbaji dhahabu katika Mgodi wa North Mara, wilayani Tarime, mkoani Mara.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari inayopatikana pia kwenye tovuti yake, tume hiyo imesema uchunguzi wake kuhusu malalamiko dhidi ya North Mara Gold Mine Limited umegundua mgodi huo ulitwaa ardhi yenye ukubwa wa ekari 652 katika vijiji vya Komarera na Kewanja kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za uchimbaji dhahabu.

"Hakuna ukiukwaji wowote wa haki za binadamu uliofanywa na mgodi wa dhahabu wa North Mara wakati wa zoezi la upanuzi wa eneo la uchimbaji katika vijiji vya Komarera na Kewanja wilaya ya Tarime, mkoani Mara," inasomeka sehemu ya taarifa ya THBUB.

Tume hiyo inaendelea kueleza kuwa zoezi la uthamini na utwaaji eneo husika lilifuata taratibu na lilifanyika kwa uwazi na ushirikishwaji wa pande zote; wananchi ambao walikuwa wanamiliki ardhi katika maeneo yaliyochukuliwa na mgodi, walilipwa fidia stahiki.

"Katika uchunguzi kuhusu malalamiko ya wananchi wa vijiji vya Komarera na Kewanja dhidi ya mgodi wa North Mara, THBUB imebaini kwamba mgodi wa North Mara ulitwaa ardhi yenye ukubwa wa ekari 652 katika kijiji cha Komarera kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za mgodi na zoezi la utahmini na utwaaji eneo husika lilifuata taratibu," inaeleza tume hiyo.

Tume ilipokea malalamiko dhidi ya mgodi huo na kulazimika kufanya uchunguzi ili kubaini ikiwa ni kweli hapakuwa na uzingatiaji utaratibu wakati wa utwaaji ardhi mwaka 2021 na 2022.

Shirika lisilo la kiserikali la MiningWatch la Canada ni kati ya mashirika kadhaa ya nje ya nchi ambayo yamekuwa yanaibua tuhuma za mara kwa mara dhidi ya mgodi wa North Mara ambapo safari hii linadai kulikuwa na ukiukwaji haki za binadamu katika zoezi la utwaaji eneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji dhahabu za mgodi huo.

Ofisa wa MiningWatch, Catherine Coumans amenukuliwa katika taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya shirika hilo, akidai kwamba maelfu ya watu wa jamii ya Wakurya wamehamishwa kwa nguvu kutoka katika ardhi yao ili kupisha upanuzi wa mgodi.

Coumans alidai kwamba watu wengi walihamishwa mnamo Desemba 2022, huku mchakato huo ukikiuka haki za binadamu, madai ambayo hata hivyo yalikanushwa vikali na kampuni ya Barrick Gold inayomiliki mgodi wa North Mara kwa ubia na Serikali ya Tanzania kupitia kampuni ya Twiga Minerals.

Kampuni ya Barrick Gold ambayo inakiri kupokea malalamiko hayo, imesema katika taarifa yake kwamba tuhuma hizo zimetolewa kwa nia ovu.

Imesema kwamba tuhuma hizo hazina msingi wowote kwa kuwa zilishajibiwa kwa kina kupitia taarifa mbalimbali za mgodi wa North Mara kuhusu masuala yote yanayohusiana na shughuli za uchimbaji.

Taarifa ya Barrick Gold ambayo pia inapatikana kwenye tovuti ya kampuni hiyo imesema kwamba inajivunia kazi ambayo inafanywa na North Mara Gold Mine Limited (NMGML) ya kujenga uhusiano na kuaminika miongoni mwa wananchi wanaoishi jirani na mgodi huo.

"North Mara Gold Mine Limited inafanya kazi kwa kushirikiana na mashirika mengi ya kiraia ya ndani na ya nje, kwa sera ya milango wazi na hufanya ziara na mikutano angalau kila robo mwaka, ikiwa ni pamoja na miradi maalum, kama vile mapitio ya mifumo ya malalamiko na uhamasishaji, au elimu na uhamasishaji kwenye jamii," inasomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Mgodi wa North Mara unaelezwa kuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi kwa wananchi wanaozunguka mgodi huo na taifa kwa ujumla.

Mbali na gawio la faida inayotokana na mauzo ya dhahabu nje ya nchi, Serikali ya Tanzania hunufaika na kodi na tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za uchimbaji dhahabu katika mgodi huo.

Manufaa mengine ya moja kwa moja yanayotokana na shughuli za mgodi huo ni pamoja na kampuni mbalimbali zinazomilikiwa na wazawa kushiriki katika mnyororo wa thamani kwa kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali mgodini huko kupitia mfumo unaolenga kuwawezesha Watanzania kunufaika na sekta ya madini, maarufu 'Local Content'.

Kwa mujibu wa Meneja Mkuu wa Mgodi wa North Mara, Apolinary Lyambiko, takribani kampuni 118 zinazomilikiwa na wazawa zimesajiliwa kwa ajili ya kuuza bidhaa na au kutoa huduma mbalimbali mgodini hapo.

Hatua hiyo imewezesha kampuni hizo kuajiri takribani watu 1,144, wengi wao wakiwa na wenyeji wanaotoka vijiji vinavyozunguka mgodi huo.

Mpango wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) pia ni miongoni mwa manufaa wanayoyapata wananchi wa Tanzania kutoka katika mgodi huo wa North Mara Gold Mine ambao hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kugharimia shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mathalani, takwimu zinaonesha kwamba kwa mwaka 2023 pekee, mgodi wa Barrick North Mara ulitumia zaidi ya Sh. bilioni saba kugharamia utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini.

Meneja Mkuu wa North Mara Gold Mine Limited, Apolnary Lyambiko anasema kwamba mwaka 2024, mgodi huo unatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni tisa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Vijijini kupitia mpango wake CSR.

# WATANZANIA WAITWA MCHEZO MPYA KUSAKA MEDALI OLIMPIKI

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wametakiwa kushiriki mchezo mpya wa Kimataifa wa Kupitia Vikwazo (World Obstacle Adventure Racing), unaoanzishwa hapa nchini ili kupata fursa za kuiwakilisha nchi katika michuano mbalimbali ya kimataifa ikiwamo michezo maarufu ya Olimpiki.

Mchezo huu umekuwa ukijipatia umaarufu duniani ikiwa ni pamoja na barani Ulaya ambapo kuna michuano mbalimbali inafanyika.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo ya vitendo yanayoendelea katika Mbuga ya Pande (Pande Game Reserve), iliyopo Dar es Salaam, Mratibu wa mafunzo hayo, Abdallah Chapa, alisema mchezo huo unajizolea umaarufu na ni moja ya michezo shindani katika michuano ya Olimpiki.

Hivyo, amewataka wanamichezo wa michezo mbalimbali wakiwamo wa riadha kujitokeza kwa wingi na kujiunga kwa sababu mchezo huo unajumuisha michezo mbalimbali ikiwamo kukimbia mbugani, kutambaa chini ya nyavu, kupanda mti kwa kutumia kamba na michezo mingine mbalimbali yenye kufurahisha.

Moja ya vikwazo pendwa vya mchezo huu, inayoonekana katika televisheni ni mchezaji kuparamia juu ya miti au bomba maalumu na kuvuka eneo ambalo akishindwa anaangukia chini ya maji.

Alisema Tanzania kuna wachezaji wenye vipaji ambao wana nafasi nzuri ya kujifunza sheria na taratibu za mchezo huu na kufanya vizuri.

"Tuna fursa za kupata medali kupitia mchezo huu na ndio maana tunatoa mafunzo kwa walimu wajue sheria na taratibu ili waweze kufundisha wachezaji watakaotuwakilisha vema katika michuano mbalimbali ya kimataifa," alisema Chapa.

Aliwashukuru wadhamini Rand Apartment, Gulamalis, Well Mark Legal, Kilimanjaro Fresh, The Green Sports Park, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori (Tawa) na Adventure Races kwa kufanikisha mafunzo hayo.

Mmoja wa washiriki hao, Ian Ochieng wa Kenya, ambaye ni mwalimu wa viungo, alisema mchezo huo utazisaidia nchi za Afrika ikiwamo Tanzania kuongeza nafasi ya kupata medali katika michuano ya Olimpiki na kutoa wito wa kufanyika maadalizi ya kutosha kwa wanamichezo.

Zaidi ya wanamichezo 50 kutoka michezo mbalimbali ikiwamo riadha na mpira wa kikapu wanashiriki kozi ya darasani na vitendo ya ukocha Dajala la Kwanza inayoendeshwa na mkufunzi Nayibe Statia kutoka visiwa vya Carribean.

Washiriki hao walishiriki michezo mbalimbali katika mbuga ya Pande iliyopo Mabwepande ukiwamo wa riadha, kupanda juu ya mti kwa kutumia kamba na kuruka uzio.



Mkufunzi wa Kozi ya Mchezo mpya wa Kimataifa wa Kupitia Vikwazo (World Obstacle Adventure Racing), Nayibe Statia, kutoka Visiwa vya Caribiani akionesha jinsi ya kucheza moja ya michezo hiyo katika hifadhi ya wanyama ya Pande mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbeya City yaanza mikakati ya kurudi tena Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City imeanza mikakati kabambe ya kuhakikisha inarejea Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kuteremka msimu wa 2022/23.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Mayanga, amesema malengo yao ni kuhakikisha wanarejea Ligi Kuu, kwani baada ya kufanya usajili mkubwa, tayari kikosi kiko kambini huku juzi kikicheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa kwenye Tamasha la Mbeya City Day, lililofanyika Uwanja wa Sokoine, Mbeya dhidi ya Real Nakonde ya Zambia na kushinda bao 1-0.

"Tupo kambini tukijiandaa na Ligi ya Champioship, ambayo msimu uliopita tulioshindwa kupanda, msimu huu tumesawazisha makosa, sasa tunaweza tukawa kwenye mazingira mazuri ya kurejea Ligi Kuu.

"Tumeshacheza mechi kadhaa za kirafiki pamoja na hii ya leo (juzi), ambayo tumecheza na timu kubwa kutoka Zambia na tumeshinda bao 1-0, tunataka kuona ubora na udhaifu wetu ili tukafanye tena masahihisho kabla ya kucheza ligi hiyo ambayo itaanza hivi karibuni, tunasubiri ratiba tu," alisema Mayanga.

Mbeya City ilipanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2013/14 na kuwa moja kati ya timu tishio, iliyokuwa na mashabiki wengi waliokuwa wakisafiri nayo kila iendapo kucheza.

Hata hivyo, ubora wa timu hiyo ulianza kupungua msimu hadi msimu na sababu kubwa ambayo mashabiki wengi waliisema ni kubadilishwa kwa viongozi kwenye Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Imeelezwa kuwa baadhi yao wamekuwa si wapenzi wa soka, hivyo timu kukosa usimamizi mzuri.

Hatimaye timu hiyo ilishuka msimu wa 2022/23, baada ya kufungwa michezo yote miwili ya ,play off', mabao 3-1 ugenini na bao 1-0 nyumbani dhidi ya Mashujaa FC iliyokuwa Ligi ya Championship, ushindi ambao uliipa tiketi timu hiyo ya Kigoma kupanda Ligi Kuu.

# JKT Tanzania waifuata Kagera Sugar mapema

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha JKT Tanzania leo kinatarajia kuanza safari kuelekea mkoani Mwanza kwa ajili ya kwenda kuweka kambi ya muda mfupi kabla ya kwenda mkoa wa Kagera kukutana na Kagera Sugar ifikapo Septemba 16, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema wameamua kwenda mkoani humo kwa kuwa hali ya hewa inafanana na ya Kagera.

"Tumeamua kuanza safari yetu mapema ili wachezaji waweze kuzoea hali ya hewa, tutakapofika Kagera wasipate tabu vile vile tutapunguza uchovu wa safari kwa kuwa kutoka Mwanza kwenda Kagera si mbali," alisema Ally.

Kocha huyo alisema mchezo wao wa juzi wa kirafiki dhidi ya Simba ulimsaidia kuangalia mapungufu ya kila mchezaji ambapo amekiri kuyafanyia kazi kabla ya kukutana na Kagera Sugar.

Alisema kwa upande wake ulikuwa mchezo wa kupima wachezaji na kudai wamejifunza vitu vingi kutoka kwa wachezaji wa Simba kutokana na uzoefu waliokuwa nao.

Kuhusu hali za wachezaji alisema mpaka sasa hajana majeruhi kikosini zaidi ya Charles Ilanfya ambaye alipewa mapumziko ya wiki mbili baada ya kuuumia walipokutana na Azam FC Agosti 28, mwaka huu, mchezo waliocheza Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo.

# Rehema aahidi taji michuano tenesi Poland

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Tenesi kwa watu wenye ulemavu, Rehema Selemani, keshokutwa, Jumatano anatarajia kukwea pipa kuelekea nchini Poland tayari kwenda kumenyana kwenye mashindano ya Dunia yatakayoanza Septemba 12-19, mwaka huu, imethibitishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha wa mchezaji huyo, Riziki Salum, alisema hana wasiwasi ya kutofanya vizuri kwa mchezaji wake huyo kutokana na aina ya mazoezi anayoendelea kumpa kwenye viwanja vya Klabu ya Gymkhana, Posta jijini Dar es Salaam.

"Rehema amepata nafasi hiyo baada ya kukidhi vigezo vilivyokuwa vinahitajika, ninaamini atakwenda kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kupitia mashindano hayo," alisema Salum.

Kwa upande wake Rehema alisema amejiandaa vizuri kuhakikisha anakwenda kufanya vema katika mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa.

"Nimejiandaa vizuri kuhakikisha nakwenda kuipeperusha vema bendera ya taifa katika mashindano hayo ambayo naamini yatakuwa na upinzani mkubwa," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND MKATABA MPYA
MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kukubaliana na mkataba mpya ambao utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi. (***Marca***)

### SALIBA ATAKIWA MADRID
REAL Madrid inalenga kumnunua mlinzi wa kati wa Arsenal na Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 23. (***Fichajes***)

### HOWE AMTAKA ANTONY
KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe anafikiria kumnunua winga wa Manchester United na Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, ikiwa dili la mshambuliaji wa Nottingham Forest na Sweden, Anthony Elanga (22), halitatimia. (***Caught Offside)***

### GUEHI AWANIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United itajaribu kumsajili mlinzi wa Crystal Palace, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, katika mkataba wa bei nafuu Januari wakati atakapokuwa amebakiza miezi 18 katika mkataba wake, lakini The Eagles hao wataendelea kushikilia hesabu yao ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa England. (***Football Insider***)

### MUSIALA AITAMANI EPL
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Jamal Musiala, ambaye anaivutia Manchester City, hajakataa kuhamia Ligi Kuu England. Mkataba wa sasa wa winga huyo wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 21, utakamilika Juni 2026. ***(Welt Am Sonntag, via Goal)***

### TAH KUONDOKA LEVERKUSEN
BEKI wa Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 28, amesema hataongeza mkataba wake na Bayer Leverkusen ambao utaendelea hadi msimu wa majira ya joto 2025, na amethibitisha kuwa Bayern Munich walikuwa miongoni mwa klabu zilizotaka kupata saini yake msimu wa majira ya joto. (***90 min***)

### RABIOT AWAPOTEZEA WATURUKI
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, ni mchezaji huru baada ya kuondoka Juventus, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hana nia ya kuhamia katika klabu moja nchini Uturuki. (***Fabrizio Romano)***

### VAN DIJK NA MKATABA
LIVERPOOL ina nia ya kumpa mkataba mpya mlinzi wa Uholanzi, Virgil van Dijk mwenye umri wa miaka 33, ili kuongeza muda wake wa kusalia Anfield zaidi ya msimu wa majira ta joto. (***Football Insider)***

### WILLIAMS NA BARCELONA
BARCELONA wanatazamiwa kufufua azma yao ya kumnunua mshambuliaji wa Athletic Bilbao, Nico Williams mwenye umri wa miaka 22, raia wa Hispania. (***Sport)***

### MOUNRIHO AMTWAA MEDINA
KLABU ya Fenerbahce inayonolewa na Jose Mourinho imekubali kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Cristian Medina mwenye umri wa miaka 22, kutoka Boca Juniors katika dirisha la Januari. (F***abrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GREALISH, RICE WAKUTANA NA KITU KIZITO HUKO IRELAND

**DUBLIN,** Ireland

DECLAN Rice na Jack Grealish walipuuzilia mbali mapokezi yao ya kuzomewa mjini Dublin wakati kila mmoja akifunga bao katika ushindi wa England wa mabao 2-0 dhidi ya Jamhuri ya Ireland kwenye Ligi ya Mataifa ya Uefa Jumamosi na kusema hawana baya lolote zaidi ya heshima kwa nchi hiyo ambayo ni asili yao na waliwahi kuichezea katika ngazi ya Timu za Taifa za Vijana.

**Rice aliichezea Ireland katika kiwango cha vijana na alicheza mechi tatu za wakubwa kwa nchi hiyo kabla ya kubadili utii wake na kuichezea England, uamuzi ambao mashabiki wengi wa Ireland hadi sasa wamekataa kuukubali.**

Huku kila akigusa mpira alikuwa akizomewa na sehemu kubwa ya mashabiki hao wa nyumbani, Rice hakujali na aliipa uongozi England kwa bao la kwanza, lakini alichagua kutoshangilia.

**Sina neno baya la kusema na ninawatakia kila la heri kama nifanyavyo mara zote...**

"Bibi na Babu yangu kwa upande wa baba yangu wote ni Wa-Ireland, wameshakufa na hawapo tena kwa hivyo, nadhani kusherehekea bao kungekuwa ni kukosa heshima, sikutaka kufanya hivyo," alisema Rice akiiambia Sky Sports baada ya mchezo huo.

"Nilikuwa na wakati mzuri sana wa kuichezea Ireland, katika kikosi cha kwanza, chini ya umri wa miaka 19, na chini ya umri wa miaka 21, zilikuwa kumbukumbu nzuri ambazo bado zinaishi na mimi.

"Sina neno baya la kusema na ninawatakia kila la heri kama nifanyavyo mara zote."

Kwa upande wa Grealish, ambaye alifunga bao la pili la England, pia aliichezea Ireland katika timu za vijana na hakushangazwa na hali hiyo ya kuzomewa kutokana na kubadili upande ukubwani.

"Ni kile ambacho mimi na Declan tulitarajia. Hatuna chochote kibaya cha kusema, sote tulifurahia wakati wetu tulipokuwa tukichezea Ireland," alisema Grealish akiiambia ITV.

"Hakika nilifanya hivyo, na mimi famila yangu yote inatoka hapa Ireland, kwa hivyo hakuna damu mbaya kutoka upande wangu."

Grealish aliachwa nje ya kikosi cha Gareth Southgate kilichoshiriki Euro 2024, lakini alifaidika zaidi na kuondolewa kwake na kocha wa muda, Lee Carsley ameamua kumuita tena.

"Msimu wa majira ya joto ulikuwa moja kati ya mibaya zaidi maishani mwangu kwa sababu huwezi kuona kinachotokea mbele yako," alisema Grealish.

"Ilikuwa ngumu, lakini imenipa azimio zaidi kurejea.

"Ilimaanisha kila kitu, kwenda tu kwa mashabiki mwishoni na kuwasikia wakishangilia jina langu."

Kocha huyo, Carsley yeye pia ni mchezaji wa zamani wa Kimataifa wa Ireland.

## HABARI MICHEZO



# ODEGAARD: MATAJI YATAIFANYA ARSENAL KUWA KLABU BORA

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Martin Odegaard, anataka mataji na ili kuonesha kwamba, 'Washikabunduki' hao ndio klabu bora kwake.

Odegaard ametimiza uwezo wake wa kuwa mmoja wa viungo wakuu duniani tangu ahamie London Kaskazini kutoka Real Madrid mwaka 2021, na kuichezea Arsenal mechi 156 hadi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, anatazamiwa kuwa baba katika miezi ijayo, na katika mahojiano na TV2, alieleza jinsi anavyoridhika na nyanja zote za maisha yake.

"Ninahisi nimeimarika katika maisha yangu sasa. Najihisi niko kwenye klabu bora na niko sawa nyumbani pia. Kwa hivyo sasa ninahisi kuwa mambo yako sawa," alisema.

"Kitu pekee kinachokosekana ni sisi kuanza kushinda mataji na Arsenal na kufanikiwa kutwaa ubingwa."

Arsenal wamekaribia kwa uchungu kumaliza kusubiri kwao kwa muda mrefu kwa taji la Ligi Kuu England katika misimu miwili iliyopita, lakini walifungwa walishindwa mbele ya Manchester City.

Washikabunduki hao hawajashinda taji hilo tangu msimu wao wa 'Invincibles' wa 2003/04, ambao ulikuja katika uwanja wao wa zamani wa Highbury.

Odegaard pia hana taji kubwa kwa jezi za Arsenal baada ya kujiunga nao miezi kadhaa kutokana na kutwaa taji lao la mwisho - Kombe la FA 2019/20.

# Rooney afunga bao la ajabu



**MANCHESTER,** England

WAYNE Rooney alirudia ubora wake wa enzi akicheza soka la kulipwa na kuifungia Manchester United kwa mkwaju mkali wa faulo katika mchezo wa hisani wa magwiji wa timu hizo dhidi ya Celtic kwenye Uwanja wa Old Trafford, Jumamosi.

Mpira wa adhabu uliopigwa kwa mguu wa kulia wa Rooney ulipaa hadi kona ya juu kuthibitisha kwamba bado ana uwezo mkubwa licha ya kuwa na bonge na kitambi baada ya Darren Fletcher kuchezewa vibaya na Joe Ledley.

Mchezo ulimalizika kwa sare ya bao 1-1, baada ya Gary Hooper kusawazisha wageni, na Celtic wakashinda kwa mikwaju ya penalti 5-4.

"Ulikuwa wakati maalum kurejea Old Trafford leo kwa mchezo wa magwiji, na yote ni kwa sababu nzuri," alisema Rooney baada ya mechi.

"Ilikuwa nzuri kucheza hapa tena.

"Mfuko wa Hisani wa Manchester United unafanya kazi nzuri na inahusika kwa muda mrefu, kuona kazi inayofanya moja kwa moja, wakati wowote tunaweza kutoa kujaribu kusaidia, daima ni nzuri kufanya hivyo. Ni sababu kubwa.

"Ni muhimu kwamba tuendelee kufanya kile tunachoweza, wakati tunaweza, kuunga mkono Mfuko huu wa Hisani na kuendelea kuweka tabasamu kwenye nyuso za watoto."

Kikosi cha wachezaji 11 cha Man United pia kilikuwa na washindi wa taji la Ligi Kuu England, Ronny Johnsen, Mikael Silvestre, Michael Carrick, Antonio Valencia na Dimitar Berbatov.

Paul Scholes, Nicky Butt na Denis Irwin walikuwa miongoni mwa wachezaji wa akiba waliocheza wakitokea benchini, huku Bryan Robson akiwa kocha.

## Ancelotti awaonya Mbappe, Endrick

**MEXICO CITY,** Mexico

CARLO Ancelotti amewaonya Kylian Mbappe na Endrick kuhusu viwango vinavyotarajiwa kila mara wanapovaa jezi ya Real Madrid.

Hatimaye Mbappe aliwasili katika mji mkuu wa Hispania msimu huu wa majira ya joto kwa uhamisho wa bila malipo, huku ngoja ya Endrick kujiunga na Madrid ikiisha baada ya kutimiza umri wa miaka 18, Julai mwaka huu.

Wawili hao tayari wameonja ladha yao ya kwanza ya fedha kama wachezaji wa Madrid walipata mafanikio kwenye Kombe la Super Cup dhidi ya Atalanta, lakini walipoteza pointi katika mechi mbili kati ya nne za kwanza za klabu hiyo kwenye LaLiga.

Mbappe alifungua akaunti yake ya mabao kwenye LaLiga kwa mabao mawili - na Madrid italenga kuwapiku wapinzani Barcelona, ambao wameshinda mechi nne kati ya nne chini ya timu mpya ya kocha Hansi Flick, wakati ligi itakaporejea.

Kocha Ancelotti, ambaye ameidhinisha uteuzi wa kushtukiza wa kocha msaidizi kutoka Stockport County, Andy Mangan, katika siku chache zilizopita, amekuwa akizungumzia kile kinachohitajika kwa kila mchezaji wa Real Madrid - ikiwa ni pamoja na Mbappe na Endrick, ambapo amesema „wanabadilika vizuri sana" kwa mazingira yao mapya.

"Real Madrid ina viwango vya juu sana kwa sababu ndiyo klabu kubwa zaidi duniani," alisema Muitaliano huyo katika mkutano wake na waandishi wa habari nchini Mexico.

"Ina wachezaji wakubwa. Lazima uweze kuleta ubora wako katika huduma ya klabu. Hicho ndicho tunachojaribu kufanya kila mwaka. Mwaka huu, wachezaji wapya kama Kylian na Endrick wanabadilika vizuri sana. Tutakuwa na msimu mzuri wa kushindana katika mashindano yote.



"Kushinda ni ngumu sana, lakini jukumu letu ni kushindana katika kila mchezo kama kawaida katika klabu hii. Usikate tamaa na kushindana hadi mwisho. Hicho ndicho unachotakiwa kufanya unapovaa jezi ya timu ya Real Madrid."

Endrick pia ameingia kwenye orodha ya kufunga pale Madrid, akifunga bao la tatu katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Real Valladolid, lakini amewekewa kikomo cha dakika tisa pekee za kikosi cha kwanza na Ancelotti.

## HABARI MICHEZO

### Gamondi ashtukia ....

INATOKA UKURASA 24

chezaji wake wengi baada ya msimu mmoja kupita.

Alisema msimu uliopita alipata tabu sana kujua mazingira na aina ya wachezaji anaofanya nao kazi, lakini kwa sasa hana wasiwasi.

Nina furaha sana msimu huu, uliopita nilipata tabu, nilikuwa sijui vitu vingi, siwajui wachezaji ninaofanya nao kazi, siwajui aina ya wachezaji wanaocheza Ligi Kuu ya Tanzania, lakini sasa naelewa vitu vingi.

Kingine msimu huu nina wachezaji wapya sita wenye viwango vya juu ambao unaweza kufanya mabadiliko usiwe na presha yoyote, ingawa pamoja na hayo siwezi nikaahidi makubwa sana kwa sababu bado msimu ni mpya kwa mashindano yote," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

### Fadlu akamilisha...

INATOKA UKURASA 24

zwa mbele ya mashabiki wa Simba, utakuwa mzuri kwao.

"Tuna mechi ngumu dhidi ya Al Ahly Tripoli nyumbani kwao, tunacheza mbele ya mashabiki wao ambao najua watawashangilia sana, lakini sisi hivi karibuni tulicheza mechi ya majaribio dhidi ya Al Hilal ya Sudan, imetusaidia sana, ulikuwa ni mchezo mzuri na kipimo tosha kwetu, imetuonesha ambavyo tupo, najua tukifanya vema ugenini, na sisi tutakuja kucheza mechi ya marudiano mbele ya mashabiki wetu ambao wamekuwa wakitushangilia na kutusapoti sana, tutapata ushindi mbele yao," alisema.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi hicho kitaondoka nchini Jumatano kwenda Tripoli kwa ajili ya mchezo huo utakapigwa Jumapili ijayo, Uwanja wa Juni 11.

"Tutaondoka Jumatano na mchezo wetu utakuwa Jumapili, hatujataka kwenda mapema kwani tunajua mazingira ya karibuni nchi zote za Afrika, tunajua hata hali za hewa za nchini mbalimbali na tabia ya kila nchi tunazijua, kwa hiyo yale mambo ya zamani kwamba lazima tuwahi ili tuzoee mazingira sisi kwetu hayapo tena, sisi ni wenyeji sana katika soka hili," alitamba Ahmed.

# MWENDA, SINGIDA IMEISHA HIYO, ATUA KAMBINI RASMI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya mvutano wa muda mrefu, hatimaye beki Israel Mwenda amewasili kwenye kambi ya Klabu ya Singida Black Stars, imeelezwa.

Klabu hiyo, imemposti mchezaji huyo akiwa kambini huku mwenyewe akirekodiwa akisema amefika.

"Kwa sasa nipo kambini, nimefika, nipo na timu ya Singida Black Stars," alisema Mwenda kwa kifupi ambaye awali aligoma kujiunga nayo kwa madai ya kutaka amaliziwe kitita chake kilichosalia cha ada ya usajili, Sh. milioni 60.

Klabu hiyo kwenye mtandao wake wa instagram, umeposti video fupi ikimuonesha akiwa amevaa jezi ya klabu hiyo huku wakifanya naye mahojiano ambayo wanatarajiwa kuyarusha wakati wowote ule kwenye mitandao yao rasmi ya kijamii kuelezea kila kitu kilichotokea hadi pande zote mbili kumalizana na mchezaji huyo kuamua kurejea.

Dakika za mwisho za sakata hilo, klabu hiyo ilimtaka kuripoti kambini ndani ya saa 24 na wao kama klabu watamtimizia kile ambacho amekuwa akikidai.

Sakata hilo lilianza kwa Singida Black Stars kumtangaza mchezaji huyo kuwa ni mtoro na hajawasili kambini licha ya kumsajili.

Hata hivyo, mchezaji huyo aligoma akidai hawezi kwenda kambini mpaka watakapommalizia pesa yake hiyo ya usajili, baada ya awali kumpatia Sh. milioni 140, ambazo alizirejesha kwenye klabu yake ya zamani ya Simba.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, hakupinga hilo, ila alisema pesa hizo zilitakiwa kulipwa wakati akiwa tayari kambini, jambo ambalo lilipingwa na mchezaji mwenyewe ambaye alidai mmoja kati ya vipengele vya mkataba ni kummalizia pesa iliyobaki ili ajiunge na kambi.

Sakata hilo lilichukua nafasi kwenye vyombo vya habari kiasi cha wiki nzima, kabla ya jana kumalizika rasmi.

Mwenda ambaye tayari alikuwa ameshasajiliwa na Simba, aliomba kuondoka kwa kile kilichodaiwa kuwa hakutaka kucheza timu moja na beki mwenzake wa kulia, Shomari Kapombe, kwenye kikosi hicho, ambapo viongozi walimtaka aununue mkataba wake kwa Sh milioni 140 ili kuruhusiwa kuondoka.



**MIAKA 10...**

Mgeni Rasmi, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (watano kulia), akiongoza matembezi ya hiari jana kwenye maadhimisho ya Muheza Jogging Club kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, yaliyofanyika katika Uwanja wa Jitegemee wilayani Muheza. Wapili Kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina na watatu kushoto ni Mkuu wa wilaya hiyo, Zainab Abdallah. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Chipukizi yashukuru sare kwa Mlandege FC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Chipukizi FC imesema matokeo ya sare waliyopata dhidi ya Mlandege FC, hayakuwa mabaya hasa kulingana na ugumu uliopo wa michezo hii ya awali ya Ligi Kuu Zanzibar.

Mlandege FC ililazimishwa sare tasa na Chipukizi FC katika uwanja wake wa nyumbani kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Zanzibar uliochezwa juzi katika Uwanja wa New Amaan Complex.

Akizungumza baada ya kumalizika mchezo huo, Kocha Mkuu wa timu ya Chipukizi, Mzee Ali, alisema timu yake ilikosa utulivu katika dakika zote za mchezo.

Alisema walifanikiwa kutengeneza nafasi nyingi za wazi, lakini suala la umakini na utulivu ndicho kilichochangia kutopata matokeo ya alama tatu.

Alisema lakini pia kulikuwa na tatizo la kutojiamini kwa wachezaji wake wapya jambo ambalo anadhani ataanza nalo katika mchezo wake wa pili.

"Kupata sare katika mchezo huu wa kwanza hasa tukiwa ugenini si matokeo mabaya sana, japo tulijiandaa kwa ushindi, tumefanya makosa na tutayafanyia kazi mchezo ujao" alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Mlandege FC, Sabri China, alisema mpaka sasa hafahamu tatizo lilosababisha wachezaji wake kushindwa kupata matokeo chanya.

Alisema wachezaji wake walicheza kwa presha kubwa hali iliyowababishia kushindwa kufanya majukumu yao vizuri uwanjani.

Alisema makosa yalikuwa mengi katika safu ya ulinzi na ushambuliaji na kusababisha timu hiyo kushindwa kucheza vizuri hasa katika kuwadhibiti wapinzani wao.

"Hata sijajua tatizo nini, timu haikucheza vizuri kabisa, tunawajua wapinzani wetu mfumo wao ni mashambulizi kwa mpipira mirefu," alisema.

Hata hivyo, alisema watajipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wao wa pili hasa kwa wachezaji wao wapya ambao pia hawakuwa na kiwango kizuri.

Ligi Kuu Zanzibar itaendelea tena leo Jumatatu kwa kupigwa michezo miwili katika viwanja vya Amaan nje ,Annex A' kwa Mafunzo kuvaana na KMKM SC wakati katika Uwanja B, Uhamiaji ikimenyana na Junguni kutoka Kisiwani Pemba.

Michezo
Nipashe
Jumatatu Septemba 9, 2024

Odegaard: Mataji yataifanya Arsenal kuwa bora
UK. 22







Wachezaji wa Simba wakifurahia baada ya Salehe Karabaka kuifungia bao la pili wakati wakishinda 2-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya JKT Tanzania iliyopigwa juzi katika Uwanja wa KMC, Dar es Salaam. Aliyeshika maskio mbele ni Jean Ahoua, mfungaji wa bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti. **PICHA: NIPASHE**

# Gamondi ashtukia kitu mechi za Ligi Kuu, CAF

## ●●● Awaonya wachezaji huku akijisifu sasa anawajua vema wapinzani wao, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema yeye na wachezaji wake msimu huu ni lazima wapambane zaidi kwenye michuano mbalimbali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, kwani timu zote zimejiandaa kutaka kuwafunga.

Gamondi ambaye kikosi chake kinajiandaa kwenda kucheza mechi ya raundi ya Kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia, alisema amewaambia wachezaji wake kuwa wasijidangaye kuwa wapo kwenye mstari salama, badala yake kiwango kikubwa walichoonesha msimu uliopita kimewafanya kukamiwa zaidi na kila timu itakayokutana nayo kwenye Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu Tanzania.

**"Kila timu sasa inataka kuifunga Yanga, inabidi tupambane, tusijidangaye kuwa tupo kwenye mstari salama, ninawaambia haya hata wachezaji wangu, wanatakiwa kila siku waongeze juhudi na mazoezi zaidi ili tuwe bora kila kukicha kwani wenzetu nao wanaongeza ubora ili watufikie au watupite," alisema Gamondi.**

Alisema kwenye soka siku zote mwalimu ni lazima ujiongeze na kwani kuna presha ambayo inakusukuma ili ufanye vema.

„Na si kwenye soka tu, hata kwenye maisha ni lazima uwe na presha ya kusaka maisha, kuweza kulipa kodi, kutunza nyumba, kulisha watoto, kuwalipia ada, yote hii ni presha na hiyo ndiyo inakufanya uwe makini na ujitume.

"Kwa mfano sisi makocha kazi yetu ni ngumu, kosa moja la mwamuzi linaweza kubadilisha matokeo yote ya mchezo, timu ikafungwa, kocha ukajikuta huna kazi kwa kosa la mtu mwingine," alifafanua kocha huyo.

Hata hivyo, Gamondi ameelezea kufurahishwa na kufahamu tabia za wa-

INAENDELEA UK. 23

# Fadlu akamilisha mkakati kuiua Al Ahly Tripoli

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajiwa kuondoka Jumatano usiku kuelekea nchini Libya kwa ajili ya mchezo wa raundi ya kwanza Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli ya huko, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya Tanzania, Fadlu Davids, amesema kikosi rasmi kiko tayari kwa mashindano.

Juzi katika mchezo wake wa mwisho wa kirafiki, Simba ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, ambayo yaliwekwa wavuni na Jean Charles Ahoua kwa mkwaju wa penalti na Salehe Karabaka.

Baada ya mchezo huo, kocha Fadlu, alisema mwisho wa mchezo huo unaashiria kuwa sasa wapo tayari kwa mashindano ya kimataifa.

Alisema tayari wachezaji wake wamemaliza ule mzunguko wa wiki sita alizokuwa akihitaji za mazoezi, na mechi ambazo zingewafanya wawe na utimamu wa mwili kwa asilimia 100.

"Kilichobaki ni kuwasoma wapinzani tu, lakini furaha yangu kubwa ni utimamu wa mwili ambao wachezaji wangu wanao, na hii ni tofauti na ilivyokuwa kwenye michezo wa Ngao ya Jamii, ambapo wengi wao hawakuwa nao, pia hawakuwa na pumzi za kucheza kwa dakika zote, lakini sasa zile wiki sita nilizokuwa nazitaka zimekamilika na sasa tupo tayari," alisema Fadlu.

Alisema hana wasiwasi na wachezaji ambao wamekwenda kwenye timu zao za taifa kwa sababu huko nako wanacheza na baadhi yao watajiunga moja kwa moja jijini Tripoli.

Fadlu anaamini mchezo utakaokuwa mgumu kwao ni ule wa ugenini, ambao watatakiwa kucheza kwa juhudi ili kupata matokeo mazuri akiamini kuwa ule wa marudiano ambao utache-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >